
Nipashe
Jumamosi Juni 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581351
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Safari** ya kutisha kuiona Titanic ilivyoangamiza mabilionea baharini

UKURASA 17




**Wateule** sita TGL kuwania tuzo za Umahiri Uandishi wa Habari (EJAT)

UKURASA 3




UKURASA 11



# Binti aliyetoweka siku 36 apatikana kwa muuza mkaa

• **Ni** mwanafunzi ambaye Waziri Mkuu aliagiza msako...*Uk. 2*

Basi la Kilimanjaro Express Scania lenye namba za usajili T 983 AWY likiwa limeharibika mbele baada ya kugongana na gari dogo Toyota Corola lenye namba T 999 CPS katika eneo la Majengo Hedaru wilayani Same mkoani Kilimanjaro jana na kusababisha vifo vya watu wawili. **Picha ndogo:** Wananchi wakiangalia mabaki ya gari dogo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Mtoto ateketea kwa moto baada ya kufungiwa ndani, nyumba 30 zaungua

UKURASA 3



## Ajali ilivyoua mume, mke

UKURASA 2

MICHEZO MKUDE AZUNGUMZA KWA UCHUNGU UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# TIC kupata Tril. 4.3/- miradi ya kimkakati

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi iliyopewa hadhi ya kimkakati yenye thamani ya Dola bilioni 1.8 (Sh. trilioni 4.3) ambayo inatarajia kutoa ajira zipatazo 16,355.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mikataba hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alisema utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji ni kati ya TIC na miradi iliyopewa hadhi ya kimkakati na Kimkakati Mahiri na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (NISC).

Alisema miongoni mwa miradi hiyo ni wa kongani ya viwanda wa Sinotan unaotekelezwa Kwala, mkoani Pwani.

"Mradi huu unatarajia kuwa na uwezo wa kuwa na viwanda zaidi ya 200 ndani ya mradi utakapokamilika. Utakapokamilika unatarajiwa kugharimu Dola milioni 327 na kuleta ajira zipatazo 2000 za moja kwa moja na 50,000 ambazo si za moja kwa moja," alisema.

Mingine aliitaja kuwa ni mradi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero unaotekelezwa mkoani Morogoro, ukihusisha upanuzi na wa kilimo cha miwa unaogharimu Dola milioni 238.5 na kuleta ajira mpya zipatazo 1404 za moja kwa moja na 15,000 ambazo siyo za moja kwa moja.

"Mradi wa WILMAR unaotekelezwa Kihonda Morogoro, ni wa viwanda na uchakati wa nafaka na utakapokamilika unatarajiwa kugharimu Dola milioni 51.5 na kuleta ajira mpya zipatazo 360 za moja kwa moja na 1,000 ambazo si za moja kwa moja. Kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 271,000 za mchele na hivyo kupunguza mahitaji ya uagizwaji kutoka nje," alisema.

"Mwingine ni Mradi wa Upanuzi wa kiwanda cha uzalishaji wa saruji wa Lake Cement unaotekelezwa Kigamboni Dar es Salaam, ambao hadi sasa umewekeza Dola milioni 101," alisema

Teri alitaja mwingine ni wa kusindika na kuhifadhi gesi ya LPG na miundombinu ya gesi wa Oilcom unaotekelezwa Dar es Salaam unaogharimu Dola milioni 111.87 na kuleta ajira zipatazo 1600 za moja kwa moja 160,000 zitakazotokana na mnyororo wa thamani.

Aliitaja mingine ni Mradi wa Wild Flower and Oil Mills unaotekelezwa Manguanyuki Singida wa Dola milioni 24.

"Mradi wa Mufindi Paper Mills unatekelezwa mkoani Kigoma kwa ajili ya kilimo cha miwa na kiwanda ili kuzalisha sukari unagharimu dola milioni 320.

"Mradi wa Lodhia Steel unaotekelezwa Mkuranga mkoani Pwani utakaozalisha mabati ni wa Dola milioni 45, mradi wa Dangote Cement unaotekelezwa mkoani Mtwara na mradi wa Mount Meru Millers unaotekelezwa mkoani Singida," alisema.




Wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wakiendelea na shughuli zao katika eneo la Kimara Mwisho, Dar es Salaam jana, licha ya kuwapo kwa tangazo la Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, lenye ujumbe unaozuia kufanya biashara katika eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Binti aliyetoweka, apatikana kwa muuza mkaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWANAFUNZI wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Panda Hill iliyopo katika Bonde la Songwe mkoani Mbeya, Esther Mwanyilu (18), aliyetoweka katika mazingira ya kutatanisha, amepatikana akiwa nyumbani kwa muuza mkaa huku akiwa amebadili majina.

Binti huyo anadaiwa kutoweka shuleni hapo Mei 18, mwaka huu, tangu siku hiyo hakuwahi kuonekana mahali popote na wala taarifa zake hazikupatikana mpaka jana alipokutwa na makachero wa Jeshi la Polisi.

Baada ya kumtafuta kwa zaidi ya mwezi mmoja bila mafanikio, mama mkubwa wa wa binti huyo, Happy Yobo, aliyekuwa akimlea tangu akiwa mdogo, aliamua kujirekodi ujumbe wa sauti akilalamika kukosa msaada kutoka kwenye vyombo vya dola wala serikali.

Mama huyo alisambaza ujumbe huo kwenye mitandao ya kijamii, hatua iliyomfikia Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuagiza Serikali ya Mkoa wa Mbeya na vyombo vya dola kuongeza juhudi za kumtafuta mpaka apatikane.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga alisema, makachero wa jeshi hilo walipata taarifa za siri kuhusu uwapo wa binti huyo nyumbani kwa muuza mkaa huyo, Azurath Abdalah.

Alisema walipofika nyumbani kwa Azurath, walibaini kuwa binti huyo alikuwa amebadili jina na kujiita Elica, na kusababisha asibainike mapema. Walipomuhoji Azurath, alisema alimpokea binti huyo kutoka kwa mchoma mkaa ambaye anamfahamu kwa jina la baba Jose akimweleza kuwa binti huyo ni mke wake na amemuoa Morogoro na kumuomba amuhifadhi.

Kamanda Kuzaga alisema, mchoma mkaa huyo alimuomba Azurath amuhifadhi binti huyo ili amchukue baada ya siku mbili atakapokuwa amepata chumba.

"Makachero wetu walibaini kuwa yuko kwa muuza mkaa huyo ambaye anaishi jirani na Hospitali ya Ifisi, tumemuhoji mwenye nyumba aliyokuwa anaishi anasema alipelekwa na mteja wake ili amuhifadhi kwa muda akidai ni mke wake," alisema Kamanda Kuzaga.

Kamanda alisema, jeshi hilo linaendelea kufanya mahojiano na mwanafunzi huyo na mwanamke aliyekuwa amemuhifadhi wakati likiendelea kumsaka mwanamume huyo aliyekuwa amemkabidhi Azurath amuhifadhi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimwagiza Ofisa Elimu wa mkoa huo, Mwalimu Ernest Hinju, kumtafutia mwanafunzi huyo shule nyingine ili akamalizie masomo yake kwa kuwa hawezi kurejeshwa katika shule aliyokuwa akisoma awali.

Aidha, aliuagiza uongozi wa shule ya Panda Hill kupunguza adhabu kwa wanafunzi baada ya kupata taarifa kwamba wanatoa adhabu kali ya viboko kwa wanafunzi jambo linaloweza kuchangia wanafunzi kutoroka.

Aliwataka wazazi pia kukaa vizuri na watoto wao ili wazijue tabia zao na kuwarekebisha wanapoona hawaendi sawa.

"Tumemchukua baadhi ya vipimo vya awali na tumebaini kuwa kwa sasa hana ujauzito, lakini tutampima tena baada ya siku tatu ili tupate matokeo ya mwisho na tutamrejesha shuleni bila masharti yoyote," alisema Homera.

"Kwa kuwa binti huyu anasema yuko tayari kurudi shuleni, sisi serikali tunamtafutia shule nyingine ambayo ina tahasusi ya PCB, tunataka amalize kidato cha sita na atimize ndoto zake, lakini yeye mwenyewe amekataa kurejea katika shule hiyo," alisema Homera.

Pia, wataendelea kumsaidia kisaikolojia kwa kuwatumia wataalamu wa ushauri nasaha ili akirejea shuleni akasome bila kujali jambo lililotokea.

Mama mkubwa wa binti huyo, Happy alilishukuru Jeshi la Polisi na serikali kwa juhudi zilizofanyika mpaka kupatikana kwa mtoto huyo akiwa hai.

Akizungumza kwa shida, binti huyo aliiomba serikali kumshughulikia mwalimu Jimmy wa Shule ya Sekondari Panda Hill, akidai kuwa yeye ndiye anayetoa adhabu zinazowaumiza wanafunzi.

Alisema yupo tayari kurejea shuleni endapo serikali itamsaidia na atahakikisha anasoma kwa bidii ili atimize ndoto zake za maisha.

# Ajali ilivyoua ofisa Uhamiaji na mkewe

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MRAKIBU wa Uhamiaji Ofisi ya Uhamiaji Kurasini, jijini Dar es Salaam, Martin Mhagama (45) na mkewe Rehema Sekhao (40), wamefariki dunia katika ajali iliyohusisha basi la abiria mali ya Kampuni ya Kilimanjaro Express na gari dogo aina ya Toyota Corola.

Ajali hiyo ilitokea jana saa 12:00 asubuhi katika eneo la Majengo, Hedaru, Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, wakati ofisa huyo na mkewe wakitokea Dar es Salaam kuelekea Moshi.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Simon Maigwa, alitaja basi hilo kuwa ni lenye namba za usajili T 983 AWY aina ya Scania na gari dogo aina ya Toyota Corola yenye namba T 999 CPS.

"Chanzo cha ajali hiyo kinachunguzwa. Hivi sasa Jeshi la Polisi linamshikilia dereva wa basi T 983 AWY aina ya Scania kwa mahojiano zaidi. Miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Same," alisema ACP Maigwa.

Juni 21, mwaka huu, ajali nyingine iliyotokea Wilaya ya Wang'ing'ombe, Mkoa wa Njombe ikilihusisha basi la abiria mali ya Kampuni ya New Force, lilisababisha vifo vya watu saba, akiwamo mtoto wa miaka minane.

Basi hilo lenye namba za usajili T 173 DZU, lilikuwa likijaribu kulipita lori na lilishindwa na kuingia mtaroni na kupinduka katika Kijiji cha Igando kilichopo Wilaya ya Wanging'ombe.

Wakati Aprili 12, mwaka huu, huko mkoani Ruvuma, ajali nyingine iliyohusisha lori la mizigo aina ya Mitsubishi Fuso, iliyokuwa ikiendeshwa na Thobias Njovu, ilisababisha vifo vya watu 13.

Ajali hiyo ya Ruvuma ilitokea katika daraja la Mto Njoka kwenye Kijiji cha Namatui, baada ya ubovu wa barabara na utelezi kulisukuma lori hilo mtoni. Aidha, Machi 8, mwaka huu, ajali ya basi iliyotokea Geita, pia ilisababisha vifo vya watu wanane, akiwamo aliyekuwa Mwandishi wa Nipashe, Kanda ya Ziwa, Richard Makore (45).

# Moto waua mtoto, wateketeza nyumba 30

**Na Waandishi Wetu**

ZAIDI ya nyumba 30 zimeteketea kwa moto katika Kisiwa cha Kasalazi, Kata ya Bulyaheke Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema na kusababisha kifo cha mtoto Ashura Makelemo (4) aliyekuwa amelala baada ya mama yake mzazi kumfungia ndani na kwenda ziwani kufuata dagaa.

Imedaiwa kuwa moto huo umesababishwa na vilipuzi vilivyotokana na mafuta huku mpenzi wa mama wa mtoto huyo, Flora Kasanduku, ambaye jina lake halikutajwa akihusika na tukio hilo lililotokea majira ya saa saba usiku kwa kinachodaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Akisimulia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kasalazi, Masunga Kipolo, aliiambia Nipashe kuwa alipokea taarifa hizo saa 7.30 usiku na juhudi za kuzima moto huo kwa kushirikiana na wananchi ziliendelea licha ya moto kuwa na kasi zaidi na kusababisa kuunguza zaidi ya nyumba 30 zenye jumla ya vyumba zaidi ya 100.

Alisema wakati wakiendelea na uokoaji wa baadhi ya vitu vilivyokuwa kwenye nyumba hizo, walipata taarifa kuwa katika nyumba ambamo moto ulianzia, alikuwamo mtoto anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka minne hadi mitano aliyekuwa amefungiwa kwa kufuli ndani ya moja ya nyumba hizo.

"Kutokana na nyumba nyingi za wavuvi kujengwa kwa mbao na mabanzi ndiyo sababu moto uliwahi kuunguza idadi kubwa, hata hivyo, baada ya kufika katika nyumba hiyo hatukufanikiwa kumwokoa mtoto huyo kwa kuwa tulimkuta ameteketea na hatambuliki tena," alisema.

Mama wa mtoto huyo, aliiambia Nipashe kuwa wakati tukio hilo linatokea alikuwa mwaloni kununua dagaa wa biashara na aliona moshi unavuka kutoka katika eneo alilotokea na kuamua kuahirisha shughuli hiyo na kurejea nyumbani.

"Baada ya kufika mwaloni nikaona moshi wa moto ikabidi nirudi, wakati narudi ndiyo nikakuta mwanangu tayari ameteketea ndani ya nyumba, alikuwa mtoto wangu wa kike pekee niliyekuwa naye," alisema kwa uchungu.

Petro Creophasi, mfanyabiashara katika eneo hilo, alisema tukio hilo lililotokea ghafla limesababisha hasara kubwa kwa wavuvi pamoja na wafanyabiashara kwa asilimia kubwa ya makazi pamoja na mali hazikufaniwa kuokolewa.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji Wilaya ya Sengerema, Juma Ngwembe, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa kutokana na eneo hilo kuwa la kisiwani ilikuwa vigumu kufikika na kwamba hawakufanikiwa kufika kwa wakati, lakini kwa sasa wanaendelea na tathimini ya gharama za vitu vilivyoteketea.

***Imeandaliwa Na Elizabeth Seleman (Sengerema), Renatus Masuguliko na Vitus Audax (Mwanza).**

# Waandishi 6 TGL wang'ara uteuzi tuzo EJAT

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAANDISHI wa habari sita wa Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian ni miongoni mwa waandishi 91 walioingia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), kwa mwaka 2022.

Waandishi hao ni Shabani Njia, Elizabeth Kilindi, Rahma Suleiman Ali, Sanula Atanas, Agusta Njoji na Francis Kajubi ambao watashiriki katika tuzo hizo zilizoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Wengine ni Jackline Silemu (ITV), Mwajuma Hassa Rajabu (EATV) na Anna Thadei Augustino (EATV).

Baadhi ya wateule wengine ni James Daud Lerombo (TBCI), Ramadhan Kabanga Mvungi (Azam TV), Grace Elibariki Mbise (Azam TV) na Dafrosa Prosper Ngailo (Azam TV).

Pia wamo Peter Elias (Mwananchi), Eprahim Bahemu (Mwananchi), Iman Makongoro (Mwananchi), Josephine Sebastian (The Citizen) na Maria Shaban Mbwana (Mwananchi).

Akitangaza majina ya wateule hao 91 kati ya 728 kutoka vyombo mbalimbali vya habari waliowasilisha kazi zao, Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema kati ya waandishi hao, wateule 36 wanaandika kwenye magazeti, 27 wanatoka mitandao ya kijamii (online), 15 kutoka radio na wanaotokea kwenye runinga ni 13.

Pia, alisema kati ya wateule hao, 44 ni wanawake 16 wakitoka kwenye magazeti, 12 mitandao ya kijamii, sita kutoka radio na 10 ni wa runinga.

Alisema wateule wanaume ni 47 kati yao 20 wanaandika magazetini, 10 wa radio na runinga ni saba huku wa mitandao ya kijamii 10.

Kajubi alisema, katika tuzo za mwaka juzi, jumla ya waandishi 59 waliteuliwa kuingia katika hatua hiyo na mwaka 2021 waandishi wa habari 60 waliingia katika king'anyiro hicho.

"Jopo la majaji saba lilikaa Bagamoyo mkoani Pwani kwa siku tisa kuanzia Juni 10 hadi 18 mwaka huu, kupitia kazi 893 zilizowasilishwa kwa ajili ya mashindano ya EJAT na limekamilisha kazi yake kwa kuwapata wateule 91.

"Jopo hilo lilitumia siku tisa badala ya nane kutokana na ongezeko la kazi 295 kutoka kazi 598 za mwaka 2021, nawapongeza majaji kwa kazi kubwa waliyofanya," alisema.

Vilevile, alisema washindi wa tuzo hizo, watajulikana katika kilele cha tuzo za EJAT kwa mwaka 2022 zitakazofanyika Julai 22, 2023 katika ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

Kiongozi wa jopo la majaji hao, Mkumbwa Ally, alisema mwaka huu, wameona kazi zilizoboreshwa ikilinganishwa na tuzo za mwaka uliopita.

Alisema katika mitandao ya kijamii wamebaini kumekuwapo na ukiukwaji wa maadili na miongozo kwenye kuripoti stori zikiwamo za watoto.

"Tumeshauri wahariri wasaidie kuongeza upelekaji wa kazi nzuri na bora wakipitisha kwa kuwa itawarahisishia kazi majaji, waangalie kazi hizo na waridhike nazo," alisema.

Alisema kazi za magazeti kulingana na vigezo vilivyowekwa nyingi ni ndefu na hazivutii wasomaji na kushauri wahariri wajitahidi kuongeza ubora wa stori.

Kadhalika kwa radio na runinga alisema kazi nyingi zimeshindwa kupenya kwenye king'anyiro hicho,kwa kuwa hazina ubunifu na viwango vinavyotakiwa kushindanishwa.




Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga akizungumza na waandishi wa habari, jijini Arusha jana, wakati akitangaza majina ya wateule 91 kati ya 728 watakaoshiriki katika Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022. Kushoto ni Mwenyekiti wa jopo la majaji wa tuzo hizo, Mkumbwa Ally. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Italia yatoa bil. 1/- kuboresha mfumo takwimu RITA

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI ya Italia imeipatia Tanzania msaada wa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuboresha programu ya kuimarisha mfumo wa takwimu na usajili wa raia nchini kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini wa mkataba huo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu Mwamba, alisema uboreshaji wa programu hiyo unalenga kuiwezesha RITA kutekeleza usajili wa raia na takwimu muhimu kwa ugatuzi wa usajili wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Dk. Natu alisema utekelezaji wa programu hiyo utafanyika katika kata 245 na vituo vya afya na hospitali 405.

"Hii itafanya jumla ya vituo vya kusajili kuwa 650 vyenye idadi ya watoto 348,391 wanaotarajiwa kusajiliwa katika wilaya 11 za Mkoa wa Tanga," alisema Dk. Natu.

Alisema shughuli zitakazo fadhiliwa kwa msaada huo zinahusisha ununuzi wa fomu za usajili, kuwapa mafunzo ya ukufunzi watumishi wa RITA makao makuu Dar es Salaam ili waweze kuwapa mafunzo watumishi wengine.

Alisema pia watawajengea uwezo na kuwapa mafunzo maofisa wa halmashauri husika.

Kadhalika, alizitaja shughuli nyingine zitakazofanywa kupitia mradi huo ni kutoa vifaa vya Teknlojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa vituo vya usajili vya mkoa na wilaya.

"Pia tutafanya majaribio na kusimika mfumo wa uchapaji unaozunguka sehemu hadi sehemu katika Mkoa wa Tanga," alisema Dk. Natu.

Kupitia kitengo cha mipango na ufuatiliaji watumishi wa RITA na serikali za mitaa watafanya utafiti wa awali kwa kukusanya takwimu za awali katika halmashauri lengwa 11.

Vyuo vilivyonufaika kupitia fedha hizo ilikuwa ni cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam.

"Hii ni miongoni mwa misaada iliyotolewa kwa serikali yetu kwa sekta mbalimbali zikihusisha ufadhili wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ambapo Serikali ya Italia ilitoa msaada wa Euro 170,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani.

Mwenyekiti wa Bodi ya RITA, Dk. Amina Msengwa alisema lengo la msaada huo ni kuhakikisha huduma za RITA zinapatikana karibu na wananchi kuanzia ngazi ya vituo vya afya ambapo mtoto anazaliwa katika ngazi za serikali za mitaa na kata.

"Uzinduzi wa mradi huu ni hatua kubwa kwa RITA kwani tunategemea watoto wote walio chini ya miaka mitano waweze kusajiliwa na kupewa vyeti."

Msaada huo umetolewa ikiwa hivi karibuni serikali hizo pia zilisaini mkataba wa mkopo nafuu wa Euro milioni 19.7 ambao umechanganywa na msaada wa Euro 200,000 kwa ajili ya kuboresha vyuo vya elimu ya juu vya ufundi vinne.




Mkurugenzi Mtendaji wa Multi Choice Tanzania, Jacqueline Woiso akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa rasmi wa dirisha la maombi kwa ajili ya msimu wa tano wa uzalishaji wa filamu barani Afrika kwa kutoa mafunzo ya umahiri kwa vijana wenye kipaji ujulikanao kama Multichoice Talent Factory. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simbachawene awaonya watumishi umma wazembe, wapenda rushwa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewaonya watumishi wa umma wazembe, wapenda rushwa na wababaishaji kuacha tabia hiyo inayokiuka utoaji huduma bora kwa wananchi.

Akizundua mikataba ya huduma kwa mteja kwa taasisi za umma jana jijini hapa, Simbachawene alisema watumishi wa umma wanapaswa kutoa huduma kwa weledi, uadilifu, uwajibikaji na uzalendo na kuwasihi wazembe, wababaishaji na wapenda rushwa kuzingatia matakwa ya mikataba hiyo.

Alisema mikataba hiyo inasaidia kubadili mitazamo ya watumishi wa umma katika utoaji wa huduma kwa kuzingatia haki, uwajibikaji, uadilifu, uzalendo, kuheshimu sheria na usawa ambayo ni misingi ya maadili katika utumishi wa umma.

"Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwenye mikataba hii upo upungufu umebainika ikiwamo kukosekana au kutohuwishwa kwa mikataba, uelewa mdogo na usimamizi usioridhisha wa utekelezaji mikataba hiyo," alisema.

Aliagiza taasisi hizo kuwa na mikata iliyo hai na kujenga uelewa kwa wateja.

"Ninaamini kuimarika kwa mifumo ya utendaji kazi serikalini hususan matumizi ya mikataba hii kutaleta mageuzi makubwa ya utendaji kutoka kwenye utendaji wa kimazoea kwenda kwenye matokeo, uwajibikaji, ufanisi katika matumizi ya rasilimali watu," alisema.

Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Juma Mkomi, alisema uzinduzi wa mikataba hiyo ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma na ni azma ya serikali kuhakikisha kila taasisi inakuwa na mkataba ili kuboresha utoaji huduma kwa umma.

# Ukwepaji kodi miradi ujenzi walalamikiwa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema kumekuwapo na ukwepaji kodi na kusababisha malalamiko dhidi ya umahiri na ujuzi wa kampuni za ndani kwa baadhi ya miradi ya ujenzi inayosimamiwa na kutekelezwa na wataalamu wa ndani.

Hayo yalisemwa juzi mkoani Morogoro na Katibu Tawala Msaidizi, Idara ya Miundombinu, Mhandisi Ezron Kilamhama, kwa niaba ya Mkuu wa mkoa huo, wakati akifungua mafunzo endelevu ya wataalamu wa majenzi yaliyoandaliwa na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Aliagiza bodi za mamlaka ya usimamizi katika sekta ya ujenzi zihakikishe wataalam wanaopewa dhamana ya kutekeleza miradi wanazingatia sheria za kodi ili serikali ipate mapato na shughuli za ujenzi ziendelee kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi.

Alisema ukaguzi unaofanywa na mamlaka za usimamizi kwenye miradi, hubaini upungufu mkubwa kwenye ubora na gharama za miradi kuwa juu. "Nimesikia katika mafunzo haya kutakuwa na mada ya mapitio kuhusu uzingatiaji wa masuala ya kodi. Mada hii itukumbushe uwajibikaji, ufuatiliaji na uzingatiaji wa nidhamu ya kulipa kodi katika kuendeleza sekta ya ujenzi," alisema.

Pia, alisema mada inayohusu ulinganifu wa gharama za ushauri kwa mujibu wa Sheria ya AQRB na Sheria ya Ununuzi wa Umma (PPRA), itasaidia kupata uelewa kuhusu ukokotoaji wa ada za ushauri kwa kuzitumia sheria hizo.

Mada inayoangalia usimamizi wa miradi katika tasnia ya ujenzi, alisema ni muhimu kwa wakati huu serikali na sekta binafsi zinatekeleza miradi mingi ya ujenzi ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi.

Alisema kama wataalamu hawatasimania vyema miradi hawataweza kupata matokeo yanayoendana na thamani ya uwekezaji unaofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Akizungumza kwa niaba ya Msajili wa Bodi ya AQRB, Kaimu Msajili wa Bodi, Mkadiriaji Majenzi, Nyaswa Kalomo, aliiomba serikali kuendelea kuajiri wataalamu waliosajiliwa na bodi katika ofisi zote za umma ili kutoa miongozo ya ujenzi kwa waendelezaji wa majengo waliopo mjini na vijijini.

"Kukosekana kwa sheria ya majengo. Sheria hii ni muhimu na ina manufaa mengi kwenye tasnia ya majengo sambamba na wataalamu kuhusika moja kwa moja kupanga, kubuni, kujenga na kutunza majengo na mazingira kwa kuzingatia usalama na afya ya watu na mali.

"Kudhibiti ubora wa vifaa ya ujenzi matumizi bora ya mifumo na miundombinu ya maji, gesi, nishati, mwanga, upepo, joto na baridi ndani na nje ya jengo pamoja na kutunza mazingira," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Ludigija Bulamile, alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa taratibu za bodi ya AQRB katika kuwanoa wataalamu ili kuwawezesha kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya ujenzi.

Alisema uchaguzi wa mada umefanywa mahusussi ili kuwakumbusha wataalamu umuhimu wa kusimania miradi ya majengo na mazingira katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku.

Dk. Bulamile alisema mada kuu ya mafunzo hayo ni Usimamizi wa Miradi katika Tasnia ya Ujenzi Tanzania ambayo itajadiliwa pamoja na mada ndogo nne.

Alizitaja mada hizo nyingine ni ushughulikiaji wa madai na masuluhisho ya migogoro katika tasnia ya ujenzi, mapitio kuhusu uzingatiaji wa masuala ya kodi na ulinganifu wa gharama za ushauri kwa mujibu wa sheria ya AQRB na PPRA.

# Wanasaikolojia kuchunguza ongezeko vitendo vya ukatili

**Na Mary Geofrey**

OFISA Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Nyamala Elisha, amewataka wanasaikolojia nchini kuchunguza tatizo la kuongezeka kwa watu wanaofanya vitendo vya ukatili wa kijinsia na mauaji licha ya vyombo vya dola kuchukua hatua.

Aidha, alitaka wanasaikolojia hao kutafuta msingi wa matatizo hayo ili kupatikana ufumbuzi wa kudumu wa matukio hayo yanayoendelea kukithiri nchini.

Elisha aliyasema hayo jana wakati akizungumza jana kwenye Mkutano Mkuu wa saba wa Chama cha Wanasaikolojia nchini (TAPA), wenye kaulimbiu 'Afya ya Akili Ustawi wa Kisaikolojia na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050'.

"Wanasaikolojia tunaomba mtusaidie kujua misingi ya haya matukio ya ukatili wa kijinsia na mauaji yanayoendelea maeneo mbalimbali nchini. Tumeona mahakama zimekuwa zikijitahidi kuchukua hatua za haraka na kuwahukumu miaka 30 jela wote wanaobainika, lakini tatizo kubwa wanafungwa watuhumiwa 15 wanaibuka wapya 15, shida ni nini," alihoji Elisha.

Aidha, alisema kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kuna matukio mengi ya ukatili yanaendelea kuibuka ambayo wanahofia kuyaripoti kwenye vyombo vya habari kwa sababu yatazua taharuki.

Alisema wanajitahidi kufanyia kazi matatizo hayo, lakini jitihada kubwa zinahitajika kutoka kwa wanasaikolojia ambao wanaweza kuelimisha jamii na kusaidia kuyapungumza.

Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Baraka Makona, alisema wanasaikolojia ni kundi muhimu ambalo linafanya kazi kwa kushirikiana na maofisa ustawi wa jamii katika kushughulikia matatizo ndani ya jamii.

Aliwataka wanasaikolojia hao kushirikiana na sekta binafsi ili kufanya kazi kwenye matatizo mengi yanayohitaji kupatiwa ufumbuzi.

Awali, Rais wa TAPO, Magolanga Shagembe, alisema lengo la mkutano huo ni kukutanisha pamoja kujadili masuala yanayowahusu na zaidi kusaidia jamii kuondokana na matatizo mbalimbali ikiwamo afya ya akili.

Alisema wanasimamia masuala ya afya ya akili, kuelimisha jamii kuhusu kuondokana na mambo yanayosababisha matatizo ya afya ya akili, kushirikiana na serikali katika miongozo ya sera katika afya ya akili na saikolojia ili kuhudumia jamii.

Wadau hao pia walipata fursa ya kujadili kwa pamoja jinsi ya kudhibiti matukio ya ukatili yanayoendelea nchini kwa kuanza na wao wenyewe kujitibu kabla na baada ya kuhudumia wateja ili kumaliza tatizo hilo ndani ya taifa.

## TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

# TANGAZO KWA UMMA

## VITUO VYA UNUNUZI WA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2023/2024

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza. NFRA hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Kwa msimu huu wa mavuno ununuzi umeanza rasmi tarehe 22 Juni, 2023.

Wakala unategemea kutumia vituo kwenye mikoa mbalimbali, ambavyo vitakua vinafunguliwa kwa kuangalia hali ya ukaukaji wa nafaka, uzalishaji wa ziada wa zao husika (mahindi na mpunga), eneo kuwa na ghala zuri la kuhifadhia nafaka, bei ya soko, usalama wa eneo, mgawanyiko wa kijiografia na kuwepo na huduma muhimu.

Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa wa Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa wa Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Manyoni), Arusha (Arusha na Manyara) na Shinyanga (Mkoa wa Kigoma na Tabora). Aidha, mpunga utanunuliwa katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Songwe, Mbeya na Tabora.

**MCHANGANUO WA VITUO VYA UNUNUZI WA NAFAKA NA BEI KWA MSIMU WA 2023/2024**

| Na. | KANDA | MKOA | WILAYA | KITUO | BEI (TZS) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | MAHINDI | MPUNGA |
| 1 | ARUSHA | Arusha | Karatu | Karatu | 900-1,000 | |
| | | Manyara | Babati | Babati | | |
| 2 | DODOMA | Dodoma | Dodoma Mjini | Kizota (Ghala kuu) | 700-800 | |
| | | Manyara | Kiteto | Kiteto | | |
| 3 | KIPAWA | Morogoro | Mvomero | Mvomero | | |
| | | Tanga | Handeni | Handeni | 800 | |
| 4 | MAKAMBAKO | Iringa | Kilolo | Ilula | 700-800 | 900-1,000 |
| | | | Iringa Vijijini | Pawaga | | |
| | | Njombe | Ludewa | Mlangali | | |
| | | | | Shaurimoyo | | |
| | | | Njombe DC | Makambako (Ghala Kuu) | | |
| | | | Wanging'ombe | Igula | | |
| | | Mbeya | Mbalali | Uturo | | |
| | | | | Madibira | | |
| | | | | Chimala | | |
| 5 | SHINYANGA | Shinyanga | Shinyanga Mjini | Shinyanga (Ghala kuu) | 750-950 | 900-1,000 |
| | | Tabora | Nzega | Bukene | | |
| | | Kigoma | Kasulu | Mvugwe | | |
| 6 | SONGEA | Ruvuma | Songea Mjini | Ruhuwiko (Ghala Kuu) | 650-700 | |
| | | | Songea Vijijini | Magagura | | |
| | | | | Mgazini | | |
| | | | Madaba Mji | Madaba | | |
| | | | Mbinga | Mbinga | | |
| | | | Namtumbo | Namtumbo | | |
| | | | Nyasa | Tingi | | |
| | | | Tunduru | Tunduru | | |
| 7 | SONGWE | Songwe | Mbozi | Vwawa (Ghala Kuu) | 650-800 | 900-1,000 |
| | | | Ileje | Isongole | | |
| | | | Momba | Kakozi | | |
| | | | Momba | Nkala | | |
| | | | Momba | Chitete | | |
| | | | Momba | Naming'ong'o | | |
| | | Mbeya | Mbeya Vijijini | Inyala | 700-800 | 900-1,000 |
| | | | Kyela | Makwale | | |
| | | | Kyela | Ngana | | |
| 8 | SUMBAWANGA | Rukwa | Sumbawanga mjini | Mazwi (Ghala Kuu) | 600-800 | |
| | | | Sumbawanga vijijini | Laela | | |
| | | | | Mtowisa | | |
| | | | Kalambo | Mwimbi | | |
| | | | Nkasi | Namanyere | | |
| | | Katavi | Mpimbwe | Majimoto | 600-800 | |
| | | | Mlele | Kibaoni | | |
| | | | Tanganyika | Sibwesa | | |
| | | | | Kasekese | | |

**Utaratibu wa Ununuzi:**
Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Bei elekezi zitakazotumika zitapangwa kwa kuzingatia umbali kutoka ghala kuu la NFRA na bei za soko katika eneo husika. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima, Wafanyabiashara na Mawakala utafanyika kupitia makubaliano yatakayofikiwa baina ya makundi hayo na Kanda za NFRA.

**Utaratibu wa Malipo:**
Malipo yote yatafanyika ndani ya siku tatu baada ya kukamilisha taratibu za kupokea nafaka.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vituo vya ununuzi, utaratibu wa ununuzi na bei katika vituo husika, wasiliana na Meneja wa Kanda/Vituo vya NFRA vilivyo karibu yako.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**
**20 Juni, 2023.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zisajili kwa matakwa na si mihemko

**HIKI** ni kipindi cha usajili kwenye ligi nyingi za soka Tanzania , ni kipindi ambacho klabu mbalimbali zinaandaa timu zao kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano ya ndani na mashindano ya kimataifa.

Ni kipindi ambacho makocha wa timu wanafanya tathimini ya wachezaji wao na kutoa ripoti kwa viongozi wao huku wakishauri maeneo gani ya kuboreshwa ili tu timu ifanye vizuri.

Kipindi hiki kocha mkuu anapewa uhuru wa kusema nini anataka kwenye timu na nini hakitaki ili tu timu ifanye vizuri kwenye msimu husika wa mashindano kuanzia yale ya ndani na nje ambayo timu inashiriki.

Kwa bahati mbaya sana hapa kwetu usajili mara nyingi unakuwa wa kihisia zaidi na si wa kimatakwa ya kikosi.

Timu zetu zinapaswa kutoka kwenye usajili wa aina hiyo, usajili wa kumfurahisha mtu, usajili wa mihemko kuwafurahisha mashabiki wa timu au wanachama.

Ifike sehemu tuwaachie wataalam wetu ambao ni makocha kufanya usajili, hapa namaanisha kufuata maoni ya kocha kwenye usajili wa wachezaji.

Kocha ndiye anayejua nani wa kumsajili na kwa sababu gani, lakini pia anajua nani wa kumuacha kwenye kikosi chake na anamuacha kwa sababu zipi.

Viongozi wa timu zetu kuanzia zile za ligi za chini mpaka ligi kuu kujenga utamaduni wa kumuachia kocha kupendekeza majina ya wachezaji anaowataka kwa ajili ya timu yake.

Kwa kufanya hivi uongozi unaweza ukawa na nguvu ya kumbananisha kocha pale timu inapofanya vibaya kwenye msimu husika kwa sababu watakuwa na sababu ya kufanya hivyo.

Sasa hivi timu nyingi zinasajili kupitia kwa viongozi, wapo makocha ambao wanaacha ripoti kwa viongozi wakiainisha mapendekezo yao kwenye usajili lakini hayafanyiwi kazi, timu ikifanya vibaya utambana vipi kocha kama huyu?.

Kufanya vizuri kwa timu kunatokana na maandalizi bora, lakini maandalizi hayo yanaanzia kwenye usajili, usajili mzuri na maandalizi bora kwenye mazoezi yanajenga timu imara yenye ushindani mkubwa.

Mashabiki na wadau wa soka tunasubiri kuona ushindani wa juu kwenye ligi yetu, ushindani wa timu na timu lakini pia ushindani wa wachezaji kwa wachezaji kwenye kikosi.

Ligi bora inategemea timu bora kwenye ligi, leo hii tunaringia ligi yetu kutajwa kuwa ni moja ya ligi bora Afrika, sifa hizi ziende kwa vitendo, tuonyeshe ubora wetu uwanjani.

Tunasisitiza klabu zetu zifanye usajili kulingana na mahitaji ya kikosi na si kufanya usajili wa mihemko, hii inapelekea timu kuwa na wachezaji ambao hawatumiki na hivyo kuingia hasara.

Lakini pia kwa wachezaji wetu, tunafahamu kipindi cha usajili ndio kipindi cha kuvuna pesa, lakini bado unapaswa kuangalia kipaji chako na si kwenda kusajiliwa kwenye timu ambayo unafahamu kabisa utaishia kukaa benchi.

Leo tunashuhudia baadhi ya timu zikiwaacha wachezaji ambao wamekaa nao kwa misimu miwili na zaidi lakini hawajawatumia, kipaji kinapotea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ligi ya Vijana U 20, lengo liwe kuibua vipaji, si kutaka ubingwa

Na Adam Fungamwango

**LIGI** ya Vijana chini ya miaka 20 imeanza wiki hii kwenye Uwanja wa Azam Complex, ikizishirikisha jumla ya timu 16 wakiwemo Mabingwa Watetezi, Mtibwa Sugar.

Timu zinazoshiriki ni zile zile ambazo kaka zao walishiriki Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika.

Kwa mujibu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya TFF, imesema kuwa ligi hiyo itaendeshwa kwa mtindo wa makundi, kila kundi likiwa na timu nne, na itachezwa hadi Juni 26 na baada ya hapo robo fainali itapigwa Juni 28 kwa timu zitakazoshika nafasi mbili za juu kwenye kila kundi, nusu fainali ikipigwa Juni 30 na fainali kuchezwa Julai 2.

Kundi A lina timu za Mtibwa Sugar, Ruvu Shooting, Mbeya City na Namungo, wakati Kundi B linaongozwa na Yanga, Polisi Tanzania, Dodoma Jiji na Prisons, huku Kundi C likiwa na timu za Coastal Union, Geita Gold, Singida Big Stars na KMC, na Kundi D linaloonekana kuwa ni la kifo kuna Simba, Azam FC, Ihefu na Kagera Sugar.

Matokeo ya mechi za mwanzo yalishuhudia Polisi Tanzania ikiichapwa mabao 4-2 dhidi ya Prisons, Yanga ikapokea kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, Simba ikatoka suluhu dhidi ya Kagera Sugar, Ruvu Shooting ikaiadabisha Namungo mabao 2-0, Mabingwa Watetezi, Mtibwa Sugar wakaanza kwa kishindo wakiibabua Mbeya City mabao 5-0, Geita Gold ikashinda mabao 2-1 dhidi ya KMC na Coastal Union ikaidungua Singida Fountaine Gate FC bao 1-0.

Mechi za mwanzo tu, mashabiki wameshuhudia mchuano mkali, timu zikipambana kwa ajili ya kuzipatia ushindi timu zao.

Kama inavyojulikana kwa watu wote wa michezo na wataalamu wa soka la vijana wanachojali sana kwa wachezaji wa umri wa miaka chini ya 17 na 20 ni vipaji vyao, uwezo na kuwaacha wacheze na kufurahia soka kama sehemu ya burudani na si vinginevyo.

Michuano hiyo ni ya kuona vipaji halisi vya wachezaji kwa sababu hawapewi mbinu sana, au kupangiwa nini cha kufanya nini cha kuacha, badala yake kuwaacha ili kuonyesha walichonacho. Kwa umri huo ukitaka kuwafundisha kama watu wazima, basi unawanyima kile walichonacho.

Mchezaji anaweza kuwa na kipaji cha kupiga chenga, na kuwaacha mabeki, ukimwambia awe anapiga chenga moja na kutoa pasi, unamnyima kuonyesha kipaji alichojaaliwa.

Kila mchezaji ana aina yake ya uchezaji aliojaaliwa, hivyo wanatakiwa kuachwa ili vionekane na kucheza kwa mfumo au maelekezo watayakuta wakiwa wakubwa.

Kwa maana hiyo napenda kuona makocha na mashabiki wote wawe wanaangalia zaidi vipaji na si nani atachukua ubingwa.

Tabia ya hadi soka la vijana watu wanatoa macho ya kutaka kuwa mabingwa inasababisha baadhi ya timu kuingiza wachezaji ambao wana umri mkubwa.

Binafsi nilipoangalia mechi zote nimeona kuna baadhi ya wachezaji hata kwa macho tu wamevuka umri wa miaka 20, au wana umri huo.

Maana ya kuwa na ligi chini ya miaka 20, ina maana wanaocheza ni kuanzia miaka 19 kurudi chini, lakini ukiwakagua kwa macho tu, utaona baadhi yao wamepita umri huo.

Tabia hii inafifisha kabisa matumaini ya kuwapata vijana wa umri sahihi kwenye soka letu kwa sababu tunapodhania kuwa ana miaka 23 au 25 na wanatakiwa waibebe nchi kenye timu ya taifa, Taifa Stars, kumbe tayari ni vibabu, wameshaanza kuzeeka.

Kwa wenzetu ni kwamba mchezaji wa miaka 16 hadi 26 wanacheza Ligi Kuu, na ndiye wale wanaotakiwa kuwa kiwango cha juu, wakishafika miaka 27 mpaka 30 wanaanza kuchoka na hata mikataba wanaanza kupewa ya mwaka mmoja mmoja.



Baadhi ya mabaharia kutoka maeneo mbalimbali nchini, wakishiriki kufanya usafi wa dakio la Mto Mirongo, Kata ya Nera, mkoani Mwanza jana, unaotiririsha maji yake kwenye Ziwa Victoria kuadhimisha siku ya mabaharia duniani ambayo kilele chake ni Juni 25 mwaka huu. Mto huo, umekuwa kero kubwa katika utiririshaji wa taka hususani za plastiki katika ziwa licha ya kuwepo zuio la muda mrefu. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Mabaharia wataka udhibiti uchafuzi Ziwa Victoria

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MABAHARIA wameomba serikali kuweka mkazo wa kudhibiti uchafuzi katika Ziwa Victoria unaotokana na taka zinazotiririshwa kupitia Mto Mirongo.

Mabaharia hao walitoa kilio chao katika Maadhimisho ya Wiki ya Mabaharia Duniani kwa serikali jana, wakati wakifanya usafi kwenye mto huo unautiririsha maji yake kwenda Ziwa Victoria.

Licha taka ngumu na nyepesi kuua mazalia ya viumbe hai majini wakiwamo samaki, husababisha pia uharibifu wa mitambo ya vyombo vya usafiri wa majini na kuwaingizia hasara wawekezaji ziwani humo.

Mabaharia hao walisema ili kudhibiti tatizo hilo kuna umuhimu wa serikali kuweka miundombinu ya taka na sheria kali zaidi.

Kaimu Meneja Mafunzo na Utoaji Vyeti kwa Mabaharia, Lameck Sondo, alisema kutokana na taka hizo kuwa tatizo, serikali inatakiwa kutenga bajeti na kuweka vifaa vya utupaji taka katika maeneo mbalimbali yanayozunguka mito inayotiririsha maji yake ziwani ili kupunguza uchafuzi huo.

"Tumebaini uwapo wa taka nyingi zikielekea ziwani na zikifika huko ni hatari kwa vyombo vyetu. Hatua hii itasaidia watu wapate pahala pa kutupa taka zao ili magari ya taka yakipita izichukue," alisema Sondo.

Mkuu wa Uzamiaji na Uokozi Kikosi cha Magendo Zanzibar KMKM, Najima Kalekwa, alisema kuna uhitaji wa kuwekwa kwa sheria ndogo katika maeneo yanayozunguka vyanzo vya maji ili kudhibiti uchafuzi ambao mara nyingi unasababishwa na shughuli za kibinadamu.

"Hali siyo nzuri katika vyanzo vya maji na hali hii inahatarisha zaidi shughuli za kiuchumi ukiwamo usafirishaji. Serikali kupitia sekta ya uhifadhi wa mazingira, inatakiwa kudhibiti uchafuzi huu kwa hali yoyote," alisema.

Kapteni Mande Mangapi, Nahodha wa Vivuko vya Kampuni ya Kamanga vinavyofanya safari zake katika Ziwa Victoria, alisema mara kadhaa wanafanya marekebisho ya vyombo vyao hususani katika maeneo ya propela ambazo husomba taka ngumu zinazosababishwa na uchafuzi ziwani humo.

"Nina imani kuwa hizi sheria ndogondogo zikiwekwa na kufuatiliwa, hakutakuwa na uchafuzi wa aina hii unaosababisha hasara kwa wawekezaji," alisema.

Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Hamidu Said, ambaye pia ni Diwani Kata ya Mirongo, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya kufanya usafi katika mito inayotiririsha maji yake Ziwa Victoria, lakini watu wanaendeleza uchafuzi kwa kificho kwenye mito hiyo.

Alisema utupaji taka ovyo siyo tu katika mito na maziwa bali, katika maeneo yote ambayo yamezuiliwa.

Pia, aliwataka wananchi kufuata utaratibu wa kuweka taka hizo katika maeneo yaliyotengwa ili zichukuliwe na magari maalum ya kuzolea taka.

# Ufaransa kusaidia zaidi bil. 1/- asasi mradi afya ya uzazi

**Na Beatrice Shayo**

UBALOZI wa Ufaransa nchini umeingia makubaliano na asasi za kiraia kutekeleza mradi wa Tanzafya ambao utagharimu Sh. bilioni 1.57 utakaohusisha utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana wenye umri wa miaka 10 hadi 24.

Mradi huo pia katika kipindi cha miaka miwili umelenga kuwafikia wasichana zaidi ya 13,000 jijini Dodoma kabla ya kusambaa katika mikoa mingine.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa utiaji wa saini na asasi tatu, Balozi Nabil Hajlaoui, alisema wanafanya kazi kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali ya Tanzania.

Alisema utekelezaji wake ni sehemu za mpango mkubwa wa mradi wa kuboresha afya za vijana unaotekelezwa na Serikali ya Ufaransa.

Pia, Serikali ya Ufaransa inatekeleza miradi mbalimbali nchini ukiwamo mradi wa kusaidia saratani unaotekelezwa kwa ushirikiano na Hospitali ya Aga Khan.

Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia afya ya watoto na vijana kutoka Wizara ya Afya, Dk. Felix Bundala, alisema mradi huo utasaidia kutatua changamoto za vijana.

"Tunazingatia maeneo makubwa yafuatayo, vijana wetu kupata taarifa sahihi kuhusu kujikinga na virusi vya Ukimwi, kujikinga na mimba za utotoni katika umri mdogo, ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto, masuala ya lishe na magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema.

Alisema watawaelimisha kutambua afya ya akili, kinga ya saratani ya mlango wa kizazi na kuhakikisha watoto wa kike wanaendelea na masomo.

Dk. Bundala alisema baada ya kuzinduliwa kwa mradi huo, watakutana na watekelezaji ili kuhakikisha taarifa zinazokwenda kwa jamii ni sahihi kadri ya miongozo ya kitaifa ili vijana wapate taarifa na huduma.

Mradi huo utafanyika jijini Dodoma kwa sababu takwimu za mimba za utotoni ni moja wapo katika eneo hilo na kadri watakavyoutekeleza watakwenda mikoa mingine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (Umati), Suzana Mkanzabi, alitaja sababu ya kuchaguliwa kwa jiji la Dodoma ni asilimia 23 ya vijana hupata mimba katika umri mdogo.

Alisema kwa kuwa jiji hilo linakua, wameona ni muhimu kuwapatia elimu sahihi ya masuala ya afya ili wajilinde mapema.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# TTB yahamasisha wadau kutangaza vivutio vya utalii

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) imewaomba wadau mbalimbali kushirikiana na serikali kutangaza vivutio vya utalii vya nchini ili kuongeza wigo wa watalii ili lengo la milioni tano lifikiwe.

Meneja Masoko wa TTB, Nassoro Garamatatu, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya safari maalumu ya kupeleka wafanyabiashara nchini China inayoratibiwa na kampuni ya GNM Cargo ya kutangaza vivutio mbalimbali vilivyoko Tanzania.

Alisema bado fursa ziko wazi kwa ajili ya kuongeza watalii nchini na endapo serikali na wadau watashirikiana itasaidia kufikia lengo lililopangwa la kuongeza zaidi idadi ya watalii nchini.

Alisema Bodi hiyo iko tayari kuwakaribisha wadau mbalimbali wenye nia nzuri ya kutangaza vivutio vya utalii ambayo pia itachangia kuongeza pato la taifa na kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuinua sekta ya utalii nchini.

"TTB imekuwa na mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii zaidi duniani ikiwamo wa utamaduni na ndiyo maana tunatoa fursa kwa wadau kwenda nchini China ili wakatangaze vivutio vyetu. Safari hii maalumu ya kitalii, itakuza zaidi mahusiano mazuri baina ya serikali za nchi hizi mbili, wadau na wananchi wao, hivyo ni eneo ambalo litaongeza fursa za kukuza utalii," alisema Garamatatu.

"Ninawaomba wafanyabiashara watakaosafiri kitalii wahakikishe wanazingatia taratibu ili uwe ni wenye vibali stahiki."

Mratibu wa safari hiyo maalumu ya kitalii nchini China, Anthony Luvanda, alisema Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki, zimeamua kuandaa safari kwa wafanyabiashara Oktoba mwaka huu ili kwenda kujifunza fursa mbalimbali za utalii nchini China, kutangaza na kuhamasisha fursa za utalii za Tanzania.

"Wachina wamekuwa wakiingia kwa ajili ya masuala mbalimbali, lakini bado idadi yao ni ndogo katika eneo la utalii, hivyo safari hii inayotarajiwa kuanza Oktoba 14-20, itaongeza zaidi hamasa kwao kuja kuona vivutio vilivyopo nchini," alisema Luvanda.

Mkurugenzi wa Masoko wa GNM Cargo, Brigita Mbano, alisema wamejipanga kusaidia wafanyabiasha na watalii wote katika safari hiyo maalumu nchini China kuwatembeza katika maeneo makubwa yenye fursa kubwa katika sekta hiyo.



Baadhi ya vijana wanaojifunza kilimo cha mviringo kwenye taasisi ya Akili Platform Tanzania, wakiweka udongo kwenye viroba, kwaajili ya maandalizi ya kilimo hicho, mjini Tabora juzi, ambacho mazao kama mahindi hupandwa ndani ya viroba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

eGA

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"


# Walimu sekondari wilaya ya Temeke wafundishwa kutumia vishkwambi

**Na Mwandishi Wetu**

WALIMU 33 wa shule za sekondari wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam, wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya vishkwambi na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), yaliyoanza Juni 12 hadi 22, mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, akizungumza wakati wa ufungaji na ugawaji wa vyeti kwa wahitimu wa mafunzo hayo, alisema elimu waliyoipata ni kichocheo kwa walimu kuendana na mageuzi na maendeleo ya viwanda.

Alisema walimu wanatakiwa kuendana na wakati ili wasipitwe na wakati kwa kuwa kizazi cha sasa hususan watoto wenye umri wa miaka sita kushuka chini, kuwa na uwezo wa kutumia simu janja ama vifaa vya kielektroniki kuliko wazazi wao, bila mafunzo ya matumizi.

"Mafunzo kama haya kwa walimu kuhusu matumizi ya vishkwambi, yanayotolewa katika mikoa ya Arusha na Ruvuma. Ni muhimu ili walimu waingie katika teknolojia ya kisasa," alisema Prof. Mdoe.

Mratibu wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Kituo cha TEHAMA (ITCoEICT) kutoka DIT, Dk. Petro Pesha, alisema kufanyika kwa mafunzo hayo kumetokana na pengo la walimu kuhusu matumizi ya vifaa hivyo.

"Tumeanzia Temeke kwa walimu 33 wa sekondari na awamu ya pili pia mafunzo haya yatatolewa kwa walimu 49 wa shule za msingi. Mikakati ni kutoa elimu kwa wilaya zote za Tanzania, pia mafunzo kama haya yanaendelea kwa walimu 200 jijini Mwanza," alisema Dk. Pesha.

Mmoja wa walimu waliohitimu mafunzo hayo, Asteria Kimambo alisema changamoto waliyoipata katika mafunzo hayo ni muda, ambao ulikuwa mfupi ikilinganisha na umuhimu wa elimu hiyo huku akiahidi kuitumia ipadavyo elimu aliyojifunza.





# Uegeshaji malori kituo cha mabasi waongeza mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

UAMUZI wa serikali ya Mkoa wa Singida kupiga marufuku malori kuegeshwa mitaani mjini Manyoni na badala yake yaegeshwe katika kituo cha mabasi Manyoni kumepandisha mapato hadi kufikia Sh. milioni 1.5 ndani ya siku nane.

Kabla ya kupiga marufuku hiyo iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, Juni 2, mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilikuwa inakusanya ushuru wa malori Sh. milioni 2.1 kwa mwezi sawa na wastani wa Sh. 70,000 kwa siku saba.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo juzi, Serukamba aliwashangaa baadhi ya madiwani wanaopinga uamuzi huo wakati umesaidia kupandisha mapato kwa halmashauri fedha ambazo zitasaidia kwa miradi ya maendeleo.

"Madiwani msitumike na watu wasiokuwa na nia njema na halmashauri, msiwe mfano mbaya katika hili suala la malori kati Mei Mosi hadi Mei 30, mwaka huu zilikusanywa Sh. milioni 2.1 kutokana na ushuru wa malori, lakini tulivyoamuru malori yawe yanaegeshwa stendi badala ya mitaani zimekusanywa zaidi ya Sh. milioni 1.5 kwa siku nane," alisema.

Katika hatua nyingine, halmashauri hiyo imeagizwa kurejesha viwanja vyenye thamani ya Sh. milioni 533 ambavyo viliuzwa kwa mkopo na kusababisha hoja ya ukaguzi iliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Serukamba alitoa siku saba halmashauri hiyo kuwapa notisi waliopewa viwanja hivyo kuvilipia na kama watashindwa wanyang'anywe na kupewa watu wengine wenye uwezo wa kuvilipia ili halmashauri ipate mapato.

Mkuu mkoa alitoa onyo kali kwa watumishi na viongozi wa halmashauri kuacha kuuza mali za umma kwa mkopo jambo ambalo alisema kuna uwezekano viwanja hivyo vimehodhiwa na watumishi hao.

"Acheni tabia ya kuuza mali za umma kwa mkopo, na inawezekana viwanja hivyo vinamilikiwa na watumishi kama madalai ili wakiuza kwa faida ndiyo walipe madeni yao," alisema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Jumanne Mlagaza, alisema baadhi ya madiwani ni miongoni mwa ambao waliochukua sehemu ya viwanja hivyo na kutovilipia hivyo kuwataka kuvilipia kabla ya matangazo ama sivyo kuvirejesha halmashauri.

# Serikali yatoa kibali ununuzi magari Jeshi la Magereza

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imetoa kibali cha kununua magari 40 kwa Jeshi la Magereza nchini ili kutatua tatizo la usafiri kwa jeshi hilo.

Akizungumza kwenye hafla ya kuzindua magari 12 ambayo tayari yamepokewa makao makuu ya jeshi hilo jijini hapa, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Mzee Ramadhan Nyamka, alisema jeshi hilo lilikuwa linakabiliwa na tatizo la magari na suala hilo linakwenda kwisha.

"Naishukuru sana serikali kutokana na kutoa fedha za kununua magari hayo, naamini utekelezaji wa kazi za magereza utazidi kuimarika," alisema.

Alisema magari yaliyowasili awali yatagawiwa katika baadhi ya magereza ya mikoa na mengine yatakayowasili yatapelekwa katika magereza ambayo bado hayajapata magari hayo.

"Naomba magari hayo yakafanye kazi za Jeshi la Magereza pekee ikiwamo yafanyiwe matengenezo kwa wakati muda wa matengenezo unapofika," alisema. Alitoa rai kwa viongozi wa magereza kuhakikisha magari hayo yanatunzwa na kufanya kazi za Magereza na siyo vinginevyo.

"Madereva mtakaokabidhiwa magari haya acheni kuendesha kwa mbwembwe barabarani," alisema.

Naye, Kaimu Kamishna wa Fedha na Mipango (SACP) wa Jeshi la Magereza, Chacha Bina alisema magari yaliyowasili awali yatagawiwa katika magereza mbalimbali hapa nchini lengo ikiwa ni kuimarisha utekelezaji wa shughuli za magereza hapa nchini.

Aliishukuru serikali kutokana na kutoa fedha hizo ambazo zimesaidia kununua magari hayo yanayogharimu zaidi ya Shilingi bilioni nne.

Kaimu Kamishna wa Utawala na Rasilimali watu wa Jeshi la Magereza (DCP), Jeremiah Katungu alisema jeshi hilo lina majukumu mawili ya kutekeleza ambayo ni kupokea wafungwa na kuwahifadhi katika usalama pamoja na kuwarekebisha.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa vya wafungwa kwa Mkuu wa Gereza la Isanga sehemu ya wanawake, SP Sifa Anyimike wakati watumishi wa tume hiyo, walipofanya ziara kwenye gereza hilo, jijini Dodoma juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma. **PICHA: TSC**

# Benki yapongezwa ubunifu huduma kisasa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu, ameishukuru Benki ya NBC kwa ubunifu mzuri wa kuanzisha huduma ya kisasa ya kidigitali 'NBC Connect' inayowezesha kampuni na taasisi mbalimbali kupata huduma salama za kibenki kwa njia ya mtandao.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Gugu aliwahimiza wateja kutumia mfumo huo mpya wa kibenki ili kurahisisha shughuli zao za kibenki.

"Uzinduzi wa NBC Connect Dodoma unawakilisha mpango mkakati wa upanuzi wa benki ya NBC ili kufikia taasisi mbalimbali na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi," alisema.

Naye, Meneja wa NBC tawi la Dodoma, Japhet Fungo, alisema huduma hiyo ni sehemu ya mchango wa benki wa kuunga mkono jitihada za serikali za kuongeza ujumuifu katika huduma za kifedha kwa makundi mbalimbali.

Alisema kupitia NBC Connect, wateja wenye kampuni na taasisi zilizopo mkoani Dodoma na maeneo ya jirani yatafanya miamala yao ya kifedha kwa urahisi zaidi na kupata uzoefu mpya.

Alisema huduma itawapa wateja uwezo wa kufanya miamala kirahisi ikiwa ni pamoja na malipo ya ndani na nje ya nchi, malipo ya serikali pamoja na ya mkupuo bila kuchukua muda kwa kutumia simu au kompyuta.

"Tunafuraha kutambulisha NBC Connect kwa wakazi wa Dodoma na maeneo ya jirani mfumo huu wa kibenki wa kidigitali ni uthibitisho wa dhamira ya kuwapatia wateja wetu huduma bora za kibenki ambazo ni rahisi, salama, na kukidhi mahitaji ya yao," alisema.

Alisema NBC Connect itatoa usaidizi binafsi kwa wateja kupitia kituo chake cha huduma kwa wateja na mameneja wa benki hiyo wanapatikana ili kuwasaidia wateja kulingana na mahitaji yao.





# Viwango kodi miundombinu kwa wageni vyalalamikiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HATUA ya Serikali ya Zanzibar kufanya marekebisho ya viwango vya kodi ya miundombinu kwa wageni wanaolala katika hoteli za Zanzibar imeibua mshtuko na malalamiko kwa wawekezaji wa sekta ya utalii visiwani humo.

Serikali kupitia bajeti yake ya mwaka 2023/24 ilitangaza marekebisho hayo na kusema kwa zaidi ya miaka minane imekuwa ikitoza kodi ya Dola moja ya miundombinu kwa mgeni anayelala katika hoteli.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, alisema kiwango hicho kimepitwa na wakati na hakiendani na mabadiliko makubwa ya kiuchumi yanayoendelea na yanayohitajika.

Alisema kiwango hicho hakijazingatia mabadiliko ya kasi ya mfumuko wa bei na thamani ya ubadilishaji wa fedha za kigeni.

Simai alisema serikali imependekeza, kodi hiyo ilipwe Dola tano kwa mgeni anayelala katika hoteli zenye hadhi ya nyota tano na nne, Dola nne kwa mgeni anayelala katika hoteli zenye hadhi ya nyota tatu au mbili. Kadhalika Dola mbili kwa mgeni anayelala katika hoteli zenye hadhi ya nyota moja na nyingine zote ambazo hazijapewa hadhi.

Waziri Simai alisema wizara yake itakaa pamoja na wawekezaji hao wa sekta ya utalii ili kuboresha huduma bora za watalii na kuongezeka kasi ya ukusanyaji kodi katika sekta hiyo.

Alisema utalii unachangia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa mapato ni lazima serikali ikusanye kodi na kupeleka maendeleo kwa wananchi ikiwamo afya, elimu na miundombinu mingine muhimu.

"Bado kuna changamoto ya idadi ya watalii wanaokuja Zanzibar na mapato yanayokusanywa, hayaendani kabisa sasa hizi fedha, lazima tuzipate, hatutaki faida, tunachotaka ni kodi ya wananchi," alisisitiza.

Kiongozi huyo pia aliwataka wawekezaji kulipa kodi kwa hiari ili kuboresha huduma za utalii na maslahi ya nchi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Uwekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI), Rahim Bhaluu, alisema mabadiliko hayo yameleta mshtuko kwa wawekezaji wa sekta hiyo.

Alisema lazima kuwapo kwa kikao cha majadiliano kati ya serikali na wawekezaji wa sekta hiyo kujadili suala hilo na kuona namna mabadiliko hayo yatakavyotekelezwa.

"Mabadiliko ya ulipaji wa kodi yametupa mshtuko mkubwa, serikali ilitakiwa kutoa muda kabla ya kutekelezwa," alisema.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Yussuph Juma Mwenda, alisema kampuni nyingi hazina uwazi katika biashara, ni vyema kuwa na uwazi katika ulipaji wa kodi.

Alisema bajeti iliyopitishwa ina mabadiliko mengi yanayowagusa wawekezaji wa sekta ya utalii ikiwamo kutoa taarifa ya wageni waliongia na kutoka hotelini i na kiasi walicholipa.

Alisema kodi hiyo itasaidia kutengeneza miundombinu ya Zanzibar ikiwamo barabara hivyo ni lazima serikali itafute fedha kuhudumia miundombinu hiyo.

Alisema ZRA imeanzisha mfumo mpya ambao utasimamia kodi Zanzibar kwa njia ya mtandao na tayari walipakodi wakubwa 180 wameshasajiliwa.



Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, Mwanaasha Khamis akichangia hoja katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Shirika Mawasiliano kuongeza kasi teknolojia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amesema uanzishaji wa Shirika la Mawasiliano Zanzibar, utaongeza kasi ya teknolojia ya mawasiliano visiwani humo.

Akizungumza jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, alisema muswada huo ni muhimu ili kwenda na wakati wa teknolojia ya mawasiliano ya ulimwengu (TEHAMA) kwa ajili ya uwekezaji.

Alisema kuwapo kwa shirika hilo kwa kiasi kikubwa kutasaidia kudhibiti matukio ya udukuzi wa mitandao na taarifa za umma na wananchi kwa ujumla.

Alisema litasaidia kuharakisha upatikanaji na matumizi sahihi ya mawasiliano ya mitandao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi, Nishati ya Baraza la Wawakilishi, Yahya Rashid Abdulla, alisema kwa kiasi kikubwa litakwenda kusaidia kukidhi mahitaji ya matumizi ya teknolojia kwa kutumia mkongo wa taifa ambao mahitaji yake ni makubwa.

Alisema maendeleo makubwa yamefikiwa ambapo mkongo wa taifa kwa sasa matumizi yake yatakwenda sambamba na maendeleo ya kibiashara kwa wateja katika kuwapatia huduma.

# Wahadhiri Zanzibar kusomeshwa nje kuendana na soko la kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU WAZIRI ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, amesema katika kuleta mageuzi ya elimu, serikali itahakikisha inawasomesha wahadhiri wa vyuo vikuu nje ya nchi ili kusaidia kutoa elimu na ujuzi wenye kiwango bora utakaoendana na soko la ajira kimataifa.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika mkutano wa wadau wa uwasilishaji wa hatua za utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) uliofanyika chuo cha utalii Maruhubi Zanzibar.

Alisema kupitia mradi huo, serikali itatoa ruzuku kwa vyuo vikuu binafsi kwa ajili ya kusomesha wahadhiri katika masuala ya afya na tiba kutokana na mahitaji makubwa ya wataalamu katika sekta hiyo.

Naibu waziri huyo alisema kupitia utekelezaji wa mradi huo, serikali itaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu na taasisi zinazonufaika kwa kutekeleza mambo mbalimbali.

"Kiasi cha Dola za Marekani milioni 329 sawa na wastani wa Sh. bilioni 752.50 zitatumika kujenga miundombinu mipya na kukarabati iliyoko ikiwamo maabara, mabweni na kuweka vifaa vya kisasa vya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) katika vyuo vikuu," alisema.

Gulam alisema Sh. bilioni 18.23 zitatumika kuhuisha na kuandaa mitaala mipya zaidi ya 290 ili kuhakikisha elimu inayotolewa inaendana na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Alisema serikali itatumia Sh. bilioni 17.83 kuboresha mazingira ya kubuni na kuunda teknolojia na kuziendeleza hasa zile zinazolenga kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi.

Akifungua mkutano huo kwa niaba ya Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa baraza hilo, Mgeni Hassan Juma alisema mradi huo utasaidia maendeleo ya elimu ya juu na kiuchumi Zanzibar.

Alisema elimu ya juu ni nguzo muhimu katika kujenga jamii yenye ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kukuza uchumi na maendeleo ya jamii.

Alisema kupitia mradi huu, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kina jukumu la kutekeleza lengo kuu la mradi kupitia program za masomo mkakati kama ambavyo ilijipangia wakati wa matayarisho ya utekelezaji wa mradi huo kitaifa.

Kadhalika, alisema kupitia utekelezaji wa maeneo hayo muhimu kuna uwezekano wa kujenga chuo kikuu chenye viwango vya kimataifa na kutoa wahitimu wenye ujuzi wa maarifa yanayohitajika katika soko la ajira.

Alisema kukamilika kwa mradi huo, kutaongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya juu kwa vijana hasa wale ambao hawakuipata au kuikosa nafasi kutokana na ushindani.

"Mradi huu unatoa fursa ya kujenga uwezo wa watafiti na kushirikiana na wadau wa ndani na nje katika kutafuta suluhisho za kisayansi na kiteknolojia kwa changamoto zinazoikabili Zanzibar na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Makame Mohamed Haji, alisema lengo la kukutana na wadau hao ni uwasilishaji wa hatua za utekelezaji wake kwa mabadiliko ya kiuchumi.

Alisema SUZA itaendelea kutekeleza shughuli zake kuu za msingi ikiwamo kufundisha, kufanya utafiti, kutoa ushauri wa kitaaluma na kutoa msaada wa kitaalamu katika jamii.

Mradi huo unaotekelezwa na serikali ya Tanzania na Zanzibar unalenga kusomesha wahadhiri 1,100 kati yao, 623 ni Shahada ya Uzamivu na 477 Shahada ya Umahiri.



## ALICIA KEYS
UKURASA 14

JUMAMOSI JUNI 24, 2023

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE



# 'THANK YOU' YENYE MASHAKA

TANGAZO la mwanamuziki mkongwe nchini, Madee, kwamba anakaa pembeni katika jukwaa la muziki limesababisha maoni tofauti kwa watu mbalimbali.

Madee amekuwa katika sekta ya burudani kwa miongo kadhaa na kuwa miongoni mwa wakongwe wanaoheshimika katika mchango wa ukuaji wa Bongo Fleva nchini.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Madee amebainisha kwamba kutokana na umri wake kuwa umekwenda ameamua kubwaga manyanga na kuwaachia vijana ambao nguvu zao ni kubwa katika kukabiliana na ugumu wa kazi hiyo.

Hata hivyo, baadhi ya watu waliotoa maoni yao kuhusu hatua hiyo, wametoa maoni tofauti kuna waliompongeza na wale walioonyesha wasiwasi wa msanii huyo kuachwa na muziki wa kileo.

Baadhi ya mastaa waliojitokeza kutoa maoni yao, walimpongeza msanii huyo kuchukua hatua hiyo, wakieleza kwamba ameacha akiwa na heshima na kuwa moja ya alama ya muziki wa Bongo Fleva.

Hata hivyo, baadhi wamedai Madee, ameingia katika mfumo wa wanamuziki wengi ambao wanatangaza kustaafu, na pale maisha yanapokuwa magumu wanarudi tena.

Wametolea mfano mwimbaji wa taarabu, Mzee Yusuph, ambaye huko nyuma alitangaza kuacha muziki, lakini aliamua kurudi tena jukwaani baada ya hali ya kimaisha kuwa mbaya.

Wengine walienda mbali kwa kueleza kuwa amechukua hatua hiyo kwa kuchelewa kwani kutokana na mabadiliko ya muziki wa sasa, hawezi kumudu kwenda nao kutokana na nguvu zake kufikia mwisho.

Aidha, kuna wale walioonyesha wasiwasi wao kuwa tamko lake linaweza kuwa kiki ya ngoma yake mpya inayokuja ambayo inawezekana jina lake linaweza kuwa 'Sitaki Tena Muziki', neno ambalo katika ujumbe wake aliliandika kwa herufi kubwa.

**BASI SAWA**

## Kusah, Maua Sama ndiyo wenyewe

MKALI wa bongo fleva, Kusah safari hii amekuja na ngoma yake nyingine mpya iitwayo, 'Wenyewe.'

Ngoma hiyo amemshirikisha



mwanadada staa kwenye tasnia hiyo, Maua Sama.

"Kama ni gari, umeliwasha limewaka, niko shwari, ukiwa kando sina mashaka." Haya ni baadhi ya maneno anayoimba Kusah kwenye wimbo ambao ambao unatarajiwa kuachiwa Juni 20.

"Vile vituko vya chumbani, virudi na ubani, vagi la tsunami, hadi nasema kunani." Haya ni maneno yanayojibiwa na Maua.

Kwenye video ya wimbo huo wasanii hao wanaimba huku wakiwa wamepakizana kwenye pikipiki aina ya vespa.


## Mbosso Khan Mi' Sitaki

Mwezi mmoja tu baada ya kuipua ngoma aliyoiita 'Amepotea' na kuteka hisia za mashabiki wengi wa muziki wa bongo fleva, msanii Mbosso kutoka WCB, kaona haitoshi, sasa kaibuka na pini nyingine matata iitwayo 'Sitaki.'

Mbosso ambaye sasa anajiita Mbosso Khan amefyatua ngoma hiyo iliyo kwenye mfumo wa video Juni 19, baada ya kuitoa mwanzo kwa mfumo wa audio, wiki mbili zilizopita.

Mbali na 'Amepotea', iliyotoka Mei 11 na kuzoa mashabiki wengi, siku mbili baadaye alitoa ngoma nyingine aliyomshirikisha Ruby, inaitwa 'Pole.'





## NDOA KWA DIAMOND SAWA NA MOTO

MWANAMUZIKI nyota wa Bongofleva, Diamond Platnumz, amepinga ushauri wa meneja wake Babu Tale wa kuwa na mke haraka.

Mmiliki huyo wa radio ya Wasafi Fm, amesema hawezi kumpiku mtu aliyeoa kwa sasa, labda pale atakapooa wake wawili.

"Babu Tale alisema nimpiku Don Fumbwe, lakini ili kumpiku labda nioe wake wawili, lakini mimi siwezi mpiku itakuwa kumkosea heshima ndugu yangu." Amesema Diamond.



## Alikiba kapata ahueni YouTube

YAWEZEKANA staa wa Bongo Fleva, Ali Kiba, amepata ahueni baada ya akaunti yake ya Youtube, kurudishwa na watekanyara wa mitandao, lakini kuna wasiwasi kawekewa mtego.

Awali akaunti hiyo ilidukuliwa na kushikiliwa na mtu aliyejiita TESLA INC, huku video zote zikiwa zimefichwa na hakuna mtu aliyefanikiwa kuzifikia.

Mbali ya video hizo kurudishwa bado kuna video moja ambayo sio ya Alikiba inaonyesha ikitumiwa na ile akaunti ya mwanzo ambayo walienda mubashara kupitia akaunti hiyo.

## MA-MISS TANZANIA WA 5 BORA KABLA YA 2000

**Na Adam Fungamwango**

PAZIA la kumsaka mlimbwende wa Tanzania kwa mwaka 2023 linatarajiwa kufunguliwa Julai mwaka huu, akisakwa mrembo atakayeshika nafasi ya malkia wa mwaka huu, Halima Kopwe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miss Tanzania Azam Mashangu anasema zaidi ya warembo 20 kutoka mikoa mbalimbali Bongo watachuana kusaka mshindi wa mwaka huu, akiamini mchuano utakuwa mkali na wa kusisimua.

Warembo hao wanatarajia kuingia kambini Juni 23, ambapo watakuwa huko kwa siku 15, ambapo pamoja na mambo mengine watakuwa wakionyesha uwezo na vipaji vyao, na watakuwa wakionyeshwa laivu mpaka siku ya shindano lenyewe.

Historia inasema Miss Tanzania wa kwanza kabisa nchini alikuwa ni Theresia Shayo, akilitwaa mwaka 1967, lakini baada ya hapo serikali ilipiga marufuku mashindano hayo kwa madai ya kimaadili, lakini yaliruhusiwa miaka ya 1990 kutokana na utandawazi kuanza kushika kasi.

Mwanamke huyo aliyeingia kwenye rekodi ya kuwa Miss wa kwanza nchini, mashindano yakifanyika kwenye Hoteli ya Kilimanjaro, Dar es Salaam Theresia, alifariki dunia Januari 26, 2007 huko Augburg Munich, nchini Ujerumani na kuzikwa huko huko alikokuwa akiishi miaka yote, akiwa na miaka 61.

Kwenye safu hii tunawaletea Ma-Miss Tanzania watano bora na maarufu waliotwaa taji mara baada ya mashindano hayo kuruhusiwa tena. Tunaowaweka hapa ni wale wa kabla ya mwaka 2000.

**Aina Maenda-1994**

Anashikilia rekodi ya kuwa Miss Tanzania wa pili tangu kuanzishwa kwa mashindano hayo nchini na wa kwanza baada ya kuruhusiwa tena ilipopigwa marufuku mara baada ya lile la kwa kwanza la mwaka 1967, lililomfanya Theresia Shayo kutwaa taji. Ilikuwa ni baada ya miaka 27, ndipo Tanzania ilipompata malkia wa urembo, Aina Maenda.

**Emily Adolf-1995**

Mwaka huo mshindi alikuwa ni mwanadada Emily Adolf, mwanafunzi wa Kidato cha Pili shule ya Sekondari Central, Dodoma.

Hata hivyo, pamoja na kutwaa taji hilo, ushindi wake ulileta malumbano makali kwa taasisi mbalimbali kupinga vikali kushirikisha wanafunzi wa shule za sekondari. Kingine walichopinga ni suala ya warembo kupitishwa wakiwa wamevalia nguo fupi.

Baraza la Sanaa la Taifa ilibidi kuweka kanuni na taratibu za kuendesha mashindano hayo na kuzuia aina hiyo ya mavazi, pamoja na wanafunzi wote wa shule za Msingi na Sekondari kutoshiriki Mashindano hayo.

**Shose Sinare-1996**

Alikuwa ni mrembo kutoka jiji la Arusha aliyefanikiwa kutwaa taji la ulimbwende la Tanzania na kuiwakilisha nchi kwenye Mashindano ya Urembo wa Dunia uliofanyika nchini India.

**Basila Mawanukuzi-1998**

Ulikuwa mwaka wa Dar es Salaam, baada ya mrembo Basila Mwanukuzi kutoka Kinondoni, kufanikiwa kuchukua taji la Miss Tanzania akifuatiwa na Nuru Doto Butamu pamoja na Diana Muhere. Baada ya kutoka kuiwakilisha nchi alianza kufanya kazi kwenye makampuni mbalimbali, Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla.

**Hoyce Temu-1999**

Dar es Salaam iliweza kutetea taji lake, lakini safari hii ilikuwa kwa mrembo aliyetokea Ilala, Hoyce Temu.

Anajulikana zaidi kama Mrembo wa Karne, au Mrembo wa Millenium, hasa ushindi wake ulikuja wakati dunia ikitoka karne ya 20 na kuingia karne ya 21, Millenium.

Ni mrembo aliyeiletea sifa sana Kamati ya Miss Tanzania na nchi kwa ujumla kwa kufanya kazi nyingi za jamii hata alipomaliza muda wake wa mwaka mmoja aliendelea kufanya kazi za kijamii akitumia jina la Miss Tanzania 1999.

**FILAMU**

# Binti Albino: Nitakulinda kama malkia

**Na Adam Fungamwango**

BINTI Albino ni filamu kali, yenye msisimko, mafunzo na ya kusikitisha, inayosimulia juu ya watu wanaotaka utajiri wasioufanyia kazi kwa kuwaua, na kukata viungo vya watu wenye ulemavu wa ngozi, wakidanganywa na baadhi ya waganga kuwa vinaleta utajiri, au vyeo.

Filamu hii imetengenezwa kwa simulizi kutoka baadhi ya watu wenye ulemavu wa ngozi kuhusu visa na mikasa iliyowakuta kwa sababu ya kuwa na hali hiyo.

Miaka 25 iliyopita baba na mama mmoja kwenye moja kati ya vijiji vya Tanzania, walimzaa mtoto wao waliyemwita Sam. Ni mtoto Albino. Malezi yake yalikuwa ya tabu, kwani wazazi hao walipata tabu ya kumlea na kumlinda kutokana na hali yake hiyo.

Mara kwa mara baadhi ya watu wabaya, wakishirikiana na waganga feki, walikuwa wanamuwinda ili wamuue kwa ajili ya kuchukua viungo vyake.

Siku moja walivunjiwa mlango na watu waliokuwa wanataka kuchukua roho ya mtoto na kwa bahati nzuri, mama na mtoto walitoka kidogo. Walimkuta baba ambaye walimpiga na kumuacha akitapatapa.

Mke aliporejea alimkuta mumewe kwenye hali mbaya. Akamwambia mkewe amevamiwa na watu waliomtaka mtoto, hivyo amkimbize haraka kwa babu yake. Mke akafanya hivyo. Huku nyuma mume alifariki. Mke aliporejea naye alikutana na watu hao, akauawa.

Sam aliishi kwa babu yake na alipofikisha umri wa miaka 25, babu yake aliamua kumwambia ukweli wote.

Sam akapatwa na hasira na kusema anataka kulipiza kisasi kwa wote waliouwa wazazi wake, na wanaosaka viungo vya Albino kwa madai ya kutaka kujipatia utajiri.

Babu alimzuia. Akamwambia hata kama anataka kulipiza lakini hawezi, kwa sababu bado hajaiva kwenye kila kitu.

Kesho yake akiwa porini aliwasikia watu ambao walikuwa wamefika kwenye kijiji hicho kwa ajili ya kuwasaka Albino baada ya kuagizwa na waganga wa kienyeji.

Akarudi mbio na kumwambia babu yake. Babu kuona hivyo, akaanza kumfundisha mjukuu wake, kulenga shabaha kwa kutumia mishale, pamoja na kumtengeneza kuwa na utimamu wa mwili.

Baada ya kuhakikisha ameiva, akamwambia sasa anaweza kupambana na mtu yeyote atakayemchokoza, au kutaka kumkamata kwa ajili ya kutaka kumuua na kuchukua viungo na hata kulipiza kisasi cha walioua wazazi wake. Anamkabidhi upinde na mishale.

Mzee mmoja jirani naye alikuwa na watoto wawili Albino, mmoja kijana na mwingine binti. Sam akawafuata na kuwaambia atahakikisha anawalinda. Akamwambia binti kuwa atamlinda kama malkia.

Kilichotokea ni historia, kwani Sam aliteketeza kundi lote hatari lililokuwa linaua Albino. Aliwateketeza waliomuua baba na mama yake, waliokuwa wanalipwa pesa kusaka Albino, waganga na wa kienyeji na hata wale waliokuwa wakisaka utajiri. Alikuwa akitumia ngumi, kareti na upende na mishale. Kijiji kikarudi kwenye hali ya amani na utulivu.



# Alicia Keys kuzunguka dunia

MWANAMUZIKI wa Marekani, Alicia Keys ametangaza kuanza kuzunguka dunia kwa ajili ya kutangaza albamu zake tano.

Grape Juice imetangaza kuwa ziara hiyo inayoitwa Keys to the Summer, itaanza Juni 28, na kuangazia kutangaza nyimbo zilizomo katika albamu zake 'Inesquecível' na 'Indolvidable' .

Keys alirekodi albamu katika miji kama vile Bogota na Sao Paolo, na baadhi ya nyimbo maarufu ni "No One" na "You Don't Know My Name".



## Nyota Hollywood kupigania tabianchi

NYOTA wa filamu za Hollywood, wamejitokeza katika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kushiriki kongamano la hali ya hewa litakalofanyika Marekani.

Msanii Jane Fonda na wakurugenzi walioshinda tuzo ya Oscar ya "Everything Everywhere All At Once" watahimiza tasnia ya burudani kukabiliana ana kwa ana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Hollywood ni tasnia yenye nguvu sana, tuko kwenye kilele cha mabadiliko ya utamaduni kwa njia nyingi"alisema Ali Weistein mkurugenzi mwenza wa mkutano huo.

Chini ya asilimia tatu ya karibu maandishi 37,000 ya TV na filamu yaliyotengenezwa tangu 2016 yalitaja maneno muhimu yanayohusiana na hali ya hewa, ni asilimia 0.6 pekee waliotumia maneno "mabadiliko ya hali ya hewa."

## Tory atoa ngoma akiwa jela

LICHA ya kuwa katika kifungo ndani ya gereza kwa kupiga risasi, Megan Thee Stallion, rapa Tory ametangaza ujio wa ngoma yake mpya.

Tory alihukumiwa kifungo Juni 13 mwaka huu baada ya kupatikana na hatia ya mauaji, kupitia ukurasa wake wa Instagram amesema atatumia chumba cha gereza kuwa ofisi yake mpya ya burudani.

Amewataka mashabiki zake kupokea ngoma hiyo inayokwenda kwa jina la Hurts Me ambayo amemshirikisha mwanamuziki Yoko Gold.





## Butcher utaweza vitasa?

RAPA mkali wa Marekani, Benny The Butcher, amewaacha midomo wazi mashabiki wake baada ya kuweka wazi kuwa ataanza kuzichapa ngumi mwezi unaokuja.

Butcher amesema Julai mosi ndiyo atapanda ulingoni katika eneo la kaskazini mwa New York, tukio hilo litakuwa na mapambano mengi.

Kwa upande wa muziki, Benny The Butcher atadondosha albamu siku chache zijazo kwenye msimu wa joto, lakini amewafahamisha mashabiki kwamba watarajie kusikia sauti mpya.

## Magixx watu wanakushangaa

Mwimbaji wa Nigeria, Magixx, amefichua jambo la kushangaza kuhusu maisha yake ya kibinafsi, huku akikiri kwamba bado ni bikira.

Katika mahojiano ya kipekee na HipTV, msanii huyo amsema maisha yake ya mapenzi tangu azaliwe hajakutana na mwanamke yeyote hadi sasa jambo ambalo linamfurahisha.

"Mimi binafsi, mimi ni bikira, kwa kweli. Unaweza kuandika mambo kutoka kwa uzoefu wako wa kibinafsi na uzoefu wa watu wengine, hivyo ningependa kujiona kama mwanasayansi ya kijamii, mwangalizi wa kijamii." Amesema Magixx







Ofisa Maendeleo ya Jamii, wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Stella Kategile akitoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, katika kata ya Mhamba wilayani humo juzi. Kutoka (kulia) ni Diwani wa kata hiyo, Fatuma Msisi, Katibu wa UWT wilaya, Hasnat Gervas na Diwani wa Viti Maalum, Mwajuma Semauya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# WWF wajitosa kutafuta suluhisho migogoro wanyama na binadamu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MFUKO wa Wanyamapori na Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), unaotekeleza mradi mkubwa wa SOKNOT Transboundary Landscape katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, umejitosa kutafuta suluhu ya kudumu ya migogoro, kati ya tembo na binadamu.

Mfuko huo unatafuta suluhu hiyo katika ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi kwa kupunguza kwa asilimia 40 ifikapo mwaka 2025.

Mradi huo unalenga kulinda na kuhakikisha wanyamapori wanaovuka mipaka na kutembeleana kutoka Kusini mwa Kenya na Kaskazini mwa Tanzania, wanaendelea kupita kwenye mapito yao waliyokuwa wanapita zamani.

Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT (Southern Kenya, Northern Tanzania), ambaye pia ni mtaalam mbobezi wa tembo, Prof. Noah Sitati, aliyasema hayo jana katika warsha ya siku mbili ya tathimini ya migogoro kati ya tembo na binadamu (HEC), iliyoandaliwa na kuratibiwa na WWF.

Akizungumza katika warsha hiyo iliyokutanisha wadau wa uhifadhi alisema malengo yao ni kupunguza migogoro hiyo katika maeneo sita yaliyolengwa. "Mkomazi ni moja ya maeneo yanayoongoza kwa migogoro kati ya tembo na binadamu nchini. Tembo wameongezeka kutoka 59 (2014) mpaka 1,200 (2019) kwa kipindi cha miaka mitano. Tembo amekuwa mnyama mharibifu na migogoro imekuwa mikubwa sana katika eneo hili la hifadhi.

"Mkomazi Ecosystem (ikolojia) ambayo inapakana na TSAVO (Hifadhi ya Taifa ya Kenya) kwa upande wa Kenya. Ukingalia ecosystem yetu ina tembo zaidi ya 16,000 upande wa Tanzania na Kenya ukijumlisha wote. Sasa ukiangalia ongezeko hilo ndiyo maana utaona migogoro imekuwa mingi katika wilaya sita za Mkinga, Korogwe, Lushoto, Same, Mwanga na Rombo," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Sitati, wataalamu hao wamekutana ili kujadili namna watakavyosaidiana na serikali kutatua changamoto hiyo kubwa, ambayo wananchi wanalalamika kushindwa kulima, njaa imekuwa kubwa na tembo wanaharibu mpaka katani.

Katika Wilaya ya Korogwe, wananchi wake wamepoteza mazao yao, baada ya tembo kuvamia na kuharibu ekari 1,251.6.

Ofisa Wanyamapori wa wilaya hiyo, Lina Nyange, alisema mwaka jana pekee, tembo walivamia vijiji 18 na kuharibu ekari 612 zilizokuwa na mazao ya wakulima.

Kutokana na uharibifu huo, alisema serikali imelazimika kuwalipa fidia au kifuta jasho, wananchi waliopoteza mazao yao, zaidi ya Sh. milioni 123.

Katika Wilaya ya Mkinga, migogoro kati ya tembo na binadamu maeneo yaliyoko pembezoni mwa ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, imesababisha hasara kubwa kwa wakulima baada ya tembo kuharibu mazao mbalimbali katika ekari 404.42 kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

Akizungumzia migogoro hiyo, Kaimu Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Mkinga, Mamboya Buge, alisema mashamba hayo yaliyokuwa na mazao ya minazi, migomba, mihogo, mahindi, choroko, korosho, nanasi, mpunga, fenesi, mikaratausi na miembe, yaliharibiwa na tembo hao mwaka 2022.

Kwa mujibu wa Buge, idadi ya watu walioharibiwa mashamba yao kwa mwaka jana walikuwa 108, mwaka 2021 walikuwa watu 19, mwaka 2020 walikuwa 43, mwaka 2019 walikuwa 12, mwaka 2018 walikuwa 14 na mwaka 2017 walikuwa 28.

# TRFA yasajili zaidi ya wakulima 70,000 Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea (TRFA), imesema idadi ya wakulima waliosajiliwa mkoani Mnyara ni 76,719 huku walionufaika na mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali wakitajwa kufikia 14,000.

Wakulima hao wamepatiwa tani 5,000 za mbolea ya ruzuku kupitia mpango maalum wa utoaji wa ruzuku hiyo.

Jana, Meneja wa TRFA, Kanda ya Kaskazini, Gothard Liampawe, akizungumza na viongozi mbalimbali wa ushirika mkoani humo katika jukwaa la maendeleo ya ushirika, alisema wakulima waliolengwa kusajiliwa walikuwa 498,669, lakini waliosajiliwa ni 76,719. "Hakuna muujiza wa kunufaika kama haujajisajili kwenye mfumo huu. Wakulima wasisubiri msimu uanze ndiyo waje kujisajili," alikumbusha.

Liampawe alionya wakulima wasidharau kanuni bora za kilimo kwa kuwa watakaodharau watapata hasara.

Meneja huyo alisema wakati wa mchakato huo wakulima wengine walikuwa wanatembea mpaka umbali wa kilomita 100 kufuata mbolea ya ruzuku na baadhi ya maofisa watendaji wa vijiji walikuwa wanatoa taarifa za uongo kuhusu upatikanaji wa mbolea hiyo.

Alisema kwa maofisa watendaji na wenyeviti wa vijiji ambao walilaumiwa kuhujumu mchakato huo, kwa sasa wakibainika watachukuliwa hatua za kisheria.

Alivitaja vikwazo vingine walivyokumbana navyo kuwa ni wakulima kutoa taarifa za uongo, kutumia vitambulisho ambavyo siyo vyao, kutotumia majina yao sahihi na baadhi yao hawakuwa wakulima.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Manyara, Absalom Cheliga, alisema Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), vina uwezo wa kununua hisa na kuwataka watumie fursa hiyo vizuri ili wanufaike na ushirika.

# Wakuu wa idara waagizwa kutafuta suluhu hoja CAG

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amewaagiza wakuu wa idara na vitengo wa Halmashauri ya Arusha, kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa kuweka viambatanisho vyote muhimu ili ziweze kufutwa.

Aliagiza kamati ya fedha na uongozi kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za halmashauri hiyo, ikiwa ni pamoja na kudhibiti upigaji wa fedha mbichi, ambao unasababisha uwapo wa hoja za CAG zinazotokana na uzembe.

Mongella alitoa maagizo hayo jana wakati wa kikao cha Baraza Maalum la Madiwani la Halmashauri hiyo lililoketi kujadili utekelezaji wa taarifa za CAG na agizo la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka wa fedha wa 2021/22.

"Hii halmashauri ina hoja 71 za CAG, zikiwamo za miaka ya nyuma 24 za sasa 47. Baadhi ya hoja zinatokana na majibu mepesi ya wakuu wa idara na wakati mwingine kutokuambatanisha vielelezo muhimu ili hoja hizo zifutwe. "Kuanzia sasa wakuu wa idara na vitengo mjibu hoja za CAG kwa umakini ili zifutwe, haiwezekani kila mwaka muwe na hoja za miaka ya nyuma wakati zinajibika," alisema.

Mongella alisema, wakuu wa idara na vitengo wakitekeleza majukumu yao kikamilifu, hoja nyingi zitakuwa ni za kisera tofauti na hivi sasa, nyingi zinatokana na wakuu wa idara na vitengo kutotimiza wajibu wao kikamilifu.

Aliagiza idara ya biashara kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato, ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki, huku akionyesha kushangazwa na mashine 82 kati ya 192 za halmashauri hiyo kuwa mbovu. "Kuna changamoto katika ukusanyaji wa mapato na ndiyo sababu mnaona kuna hoja za CAG hapa, zinazohusu idara ya biashara moja moja, lakini pia kuna utoaji wa leseni feki za baiashara.

"Mkurugenzi wa Halmashauri, Suleman Msumi, hakikisha unasimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa sababu kuna baadhi ya watumishi siyo waadilifu wanaghushi vitabu vya leseni za biashara na upigaji wa fedha mbichi kwa kisingizio cha mashine kuwa zimeharibika," alisema. Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, akizungumza katika kikao hicho, alisema changamoto kubwa ipo katika idara ya biashara, kutozingatia weledi katika kutekeleza majukumu yake.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Mfahamu Miss Bongo wa kwanza zama hizo, aliyewatengenezea njia kina Wema Sepetu

## -Alipotwaa taji, mashindano yakapigwa marufuku
## -Iliporudishwa tu, madenti, vimini, vikapigwa 'stop'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Tanzania inatarajiwa kumpata mlimbwende wake wa mwaka 2023 kuchukua nafasi ya anayeshikilia taji hilo kwa sasa, Halima Kopwe, si watu wengi wanaojua historia ya mashindano ya urembo nchini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miss Tanzania Azam Mashangu alisema zaidi ya warembo 20 kutoka mikoa mbalimbali wanaingia kambini leo na watakuwa huko kwa siku 15 kabla ya mashindano hayo kufanyika.

Wakati mashindano hayo ya kila mwaka yakifanyika, hayakupitia njia rahisi kama wengi wanavyodhani. Ni moja kati ya mashindano yaliyopita kwenye njia ngumu hadi kukubalika.

Si kwa wazazi tu kuruhusu mabinti zao, bali hata jamii nayo iliyaona ni ya kimagharibi zaidi na yamekuja kuharibu mila na desturi si za Kitanzania tu, bali za Kiafrika.

Historia ya ulimbwende Tanzania inaonyesha kuwa Miss wa kwanza kabisa ni Theresia Shayo. Huyu ndiye ameweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Miss Tanzania tangu nchi ijipatie Uhuru mwaka 1961.

Aliutwaa umalkia huo mwaka 1967, mashindano yakifanyika kwenye Hoteli ya Kilimanjaro, jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo baada ya mashindano hayo, serikali ya awamu ya kwanza ikayapiga marufuku kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kulinda maadili na utamaduni wa Mtanzania.



Mwanamke wa kwanza nchini kushinda taji la Miss Tanzania, Theresia Shayo akipita kwenye ukumbi wa Kilimanjaro, jijini Dar es Salaam kwenye mashindano yaliyompatia ushindi

Theresia, baada ya kuwa Mbongo wa kwanza kuvalishwa taji la Miss Tanzania, alibahatika kuolewa na Mjerumani aliyeitwa Chrstian Rieger na kwenda kuishi nchini Ujerumani.

Hata hivyo waliachana miaka mingi baadaye na alibaki nchini humo akiwa na mpenzi wake Tonny.

Alikuwa na nyumba yake mtaa wa Schmiedberg namba tisa katikati ya mji wa Augsburg, hadi alipofariki dunia Januari 26 mwaka 2007 kwa kile kilichoelezwa ni kansa ya tumbo akiwa na umri wa miaka 61.

Serikali ya awamu ya pili iliyaruhsu mashindano hayo kuendelea tena na ilisukumwa na utandawazi ambao ulikuwa ukishika kasi kila kukicha.

Mrembo aliyeweka rekodi ya kuwa wa pili kutwaa Umiss Tanzania ni Aina Maeda. Huyu pia ameandika rekodi ya kuwa Mbongo wa kwanza kutwaa taji hilo liliporuhusiwa tena baada ya miaka 27. Ilikuwa ni mwaka 1994 yalipofanyika mashindano ya pili ya urembo nchini, lakini yakiwa ya kwanza baada ya kuruhusiwa tena.

Mwaka uliofuata lilitaka kujitokea kama lile la mwaka 1967, lakini busara ilitumika kwa viongozi, lakini baada ya hapo kulitokea miongozo ambayo inaendelea kutumika hadi leo.

Hii ilitokana na mshindi wa mwaka 1995 ambaye hakuwa mwingine ila ni mrembo Emily Adolf.

Pamoja na furaha ya kutwaa taji hilo, lakini ilitokea kasheshe kwani alikuwa ni Mwafunzi wa Kidato cha Pili shule ya Sekondari Central, Dodoma.

Uongozi wa shule haukufurahia mwanafunzi wake kuingizwa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Ushindi wake ulileta malumbano makali pia kwa taasisi mbalimbali kupinga vikali kushirikisha wanafunzi wa shule za sekondari kwenye mashindano hayo ya urembo.

Pia wanaharakati wakapinga warembo kupitishwa majukwaani wakiwa wamevalia nguo fupi.

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) wakati huo ilibidi kuingilia kati kuweka kanuni na taratibu za kuendesha mashindano hayo na wakapiga marufuku wanafunzi wote wa Shule za Msingi na Sekondari kutoshiriki mashindano hayo.

Ndiyo mana hadi leo wanaoruhusiwa kushiriki ni kuanzia ngazi ya vyuo na kwenda juu, au wasichana kutoka mitaani, makazini na hata wafanyabiashara.

BASATA pia ikapiga marufuku warembo kupita jukwaani wakiwa wamevaa nguo fupi maarufu kama vimini. Ikumbukwe wakati huo warembo walikuwa wanapita wamevaa vimini, ikiwemo nguo za ufukweni.

Hii ndiyo sababu hadi leo Mashindano ya Urembo Tanzania huwezi kuona warembo wamevaa hivyo, au kuna wanafunzi wa msingi na sekondari. Ni kutokana na sakata hilo.

Baada ya hapo mambo yalionekana kukaa sawa na mashindano yakawa yanaendelea bila shida yoyote na kuendelea kuwatoa walimbwende ambao hadi leo wameendelea kuwa maarufu.

Shose Sinare aliutwaa umalkia mwaka 1996, kabla ya Saida Kessy kuchukua nafasi yake 1997, na 1998, Tanzania ilimpata malkia wake aliyeitwa Basila Mwanukuzi kutoka Kinondoni, Dar es Salaam.

1999, Dar es Salaam iliweza kutetea taji lake, lakini safari hii ilikuwa kwa mrembo aliyetokea Ilala, Hoyce Temu.

Anajulikana zaidi kama Mrembo wa Karne, au Mrembo wa Millenium, hasa ushindi wake ulikuja wakati dunia ikitoka karne ya 20 na kuingia karne ya 21, Millenium.

Ni mrembo aliyeiletea sifa sana Kamati ya Miss Tanzania na nchi kwa ujumla kwa kufanya kazi nyingi za jamii hata alipomaliza muda wake wa mwaka mmoja aliendelea kufanya kazi za kijamii akitumia jina la Miss Tanzania 1999.

Wakaja pia kina Happiness Magese 2001, Angela Damasi 2002, Slyvia Bahame 2003, Faraja Kotta 2004, na Nancy Sumari 2005, ambaye alifika ngazi ya juu kwenye mashindano ya ubingwa wa dunia, akifika kwenye sita bora, kabla ya Tanzania kumpata mlimbwende maarufu sana, Wema Sepetu mwaka 2006, ambaye baadaye akaja kuwa mchezaji filamu maarufu nchini.



Miss Tanzania wa mwaka 2006, Wema Sepetu mara baada ya kutangazwa kuwa mshindi, akiwa ni moja ya walimbwende maarufu zaidi nchini.



Aina Maeda (katikati) akiwa na mshindi wa pili na wa tatu kwenye mashindano ya kusaka Miss Tanzania mwaka 1994 yakiwa ya kwanza kuruhusiwa baada ya kupigwa marufuku tangu mwaka 1967.

**HABARI KIMATAIFA**

# Safari ya kutisha kuiona Titanic ilipoangamiza matajiri baharini

## -Walitumia Bilioni 3 kusafiri

**BOSTON, Marekani**

SALAMU za rambirambi zinazidi kutolewa kwa familia zilizopoteza ndugu zao baada ya nyambizi ndogo ya kitalii inayoitwa Titan, kulipuka ikiwa katika maji ya kina kirefu baharini.

Watu hao akiwamo baba na mtoto wake, walikuwa katika safari ya kitalii kwenda kuona meli ya Titanic iliyozama katika maji ya bahari ya Atlantiki miaka 110 iliyopita.

Taarifa za vifo hivyo ilitolewa na kikosi cha ulinzi wa pwani cha Marekani. Ikithibitisha kwamba watu wote watano waliokuwemo kwenye nyambizi hiyo ambayo ilipotea karibu na Titanic wamekufa.

Taarifa hiyo iliongeza kwamba chombo hicho kulilipuka katika kina kirefu cha bahari.

Tangazo hilo la kusikitisha lilihitimisha operesheni ya kimataifa ya utafutaji na uokoaji ambayo ilivutia ulimwengu tangu nyambizi hiyo ndogo ilipotoweka katika bahari ya Atlantiki Kaskazini, siku nne zilizopita.

Ofisa mkuu wa Jeshi la Wanamaji la Marekani, Rear Admiral John Mauger, aliwaambia waandishi wa habari mjini Boston, kuwa uchanganuzi ulionyesha kipande kilichopatikana kwenye sakafu ya bahari, mita 1,600 kutoka upande ilipojikita meli ya Titanic kinawiana na kulipuka kwa chemba ya gesi ya nyambizi hiyo.

"Kwa niaba ya Kikosi cha Ulinzi wa Pwani cha Marekani na kamandi yote ya pamoja, natoa rambirambi zangu za dhati kwa familia," Mauger alisema.

Ndani ya nyambizi hiyo kulikuwa na mvumbuzi kutoka Uingereza, Hamish Harding, mtaalamu wa manowari wa Ufaransa, Paul-Henri Nargeolet, tajiri wa Pakistani mwenye uraia wa Uingereza Shahzada Dawood na mwanawe Suleman, na Stockton Rush, ambaye ni mkurugenzi mtendaji wa kampuni inayoendesha nyambizi hiyo ya OceanGate Expeditions.

Katika taarifa iliyotolewa na kampuni ya OceanGate, ilielezea kuhuzunishwa na vifo vya watu hao watano na kutoa salamu za pole kwa familia na jamaa zao wakati huu wa huzuni, ikiwataja wahanga hao kuwa magunduzi halisi, walioonyesha moyo wa ujasiri na mapenzi makubwa ya kugundua na kulinda bahari za dunia.

Kikosi hicho cha ulinzi wa pwani kilitangaza mapema Alhamisi kwamba roboti ya chini ya maji, ilikuwa imegundua kipande kwenye eneo la utafutaji, na baadaye maofisa walibaini kuwa vipande hivyo vilihusisha sehemu ya mkia wa nyambizi ya Titan, pamoja na vipande vya mbele na nyuma vya ganda la kuhifadhi gesi.

Mauger alisema kikosi cha ulinzi wa pwani hakikuwa na uhakika ni lini au kwa nini nyambizi hiyo ililipuka, na alikataa kusema iwapo miili ya wahanga hao iliopolewa.

Mabaki ya nyambizi ya Titan yamegundulika mita 1,600 chini ya upinde wa mabaki ya meli ya Titanic, sawa na maili mbili chini ya uso wa bahari.

Nyambizi hiyo ndogo iitwayo Titan ilitoweka siku ya Jumapili iliposhuka kuelekea mahala ilipopata ajali meli ya Titanic, ambayo iko zaidi ya maili mbili chini ya uso wa bahari na maili 400 kutoka pwani ya Newfoundland, Canada.

OceanGate Expeditions iliwatoza abiria dola 250,000 kwa kiti kwenye nyambizi hiyo ndogo sawa na shilingi milioni 600 kwa kila mmoja.

Hata hivyo, mwaka 2018, mkurugenzi wake wa zamani wa shughuli za baharini aliibua wasiwasi kuhusu muundo wa majaribio na usiojaribiwa wa Titan.


Hamish Harding.


Paul-Henri Nargeolet.


Shahzada-Dawood.

### SAFARI YA HOFU

Jumuiya ya Kimataifa ya Titanic ilisema huenda wakati umefika wa kubadilisha safari za kwenda eneo la ajali ya Titanic kwa vyombo vinavyojiendesha vyenyewe.

Maswali ya wataalam yanaibuliwa kuhusu usalama wa maji ya chini ya bahari na jinsi yanavyodhibitiwa kufuatia ajali ya Titan, ambayo ilipasuka chini ya maji.

Titan ya OceanGate inaweza kuwa haikuhitaji kufanyiwa majaribio sawa na nyambizi zingine kwa sababu ilikuwa ikifanya kazi katika maji ya kimataifa ambapo uchunguzi wa bahari kuu haudhibitiwi, alisema Dk Simon Boxall, mhadhiri mkuu wa oceanography katika Chuo Kikuu cha Southampton.

Akizungumza katika kipindi cha BBC Breakfast, nchini Uingereza, chombo chochote ikiwamo boti, nyambizi au ROV (gari linaloendeshwa kwa kiongoza umbali), lazima kipitie ukaguzi mkali wa usalama kabla ya kuruhusiwa kuingia majini.

"Tatizo ni kwamba chombo hiki, nyambizi hii, hakikuwa chini ya mamlaka ya mtu yeyote." Alisema.

### MTOTO ALISITA

Shangazi yake Suleman Dawood, ambaye alikuwa kwenye nyambizi ya Titan na baba yake Shahzada, alisema kijana huyo mwenye umri wa miaka 19 alikuwa anasitasita kuhusu safari ya kwenda kuona ajali ya Titanic siku zilizopita.

Akizungumza na NBC News, Azmeh Dawood, dada yake Shahzada, alisema Suleman alimwambia kwamba alihisi kuogopa kuhusu safari hiyo, lakini alitaka kumfurahisha baba yake.

Walipanda nyambizi hiyo Jumapili iliyopita, ambayo ilikuwa Siku ya akina Baba huko Amerika Kaskazini.

"Siamini kilichotokea," Azmeh alisema."Ni hali ya kushangaza." alisema.

Aliongeza "Ninahisi kama nimenaswa katika hali hatari sana, na muda unayoyoma, lakini haujui utafanya nini kujinusuru, mimi binafsi napata tabu kupumua nikiwafikiria."

### SAFARI ILIKUWAJE?

Juni 17: Hamish Harding, ambaye aliendelea na safari ya chini ya bahari kwa nyambizi, alituma ujumbe kwenye Twitter kwamba misheni hiyo "inawezekana kuwa misheni ya kwanza na ya pekee iliyoendeshwa kwa nyambizi ya Titanic mnamo 2023" kutokana na msimu wa baridi kali zaidi huko Newfoundland katika miaka 40.

**Juni 18:** Titan iliondoka Polar Prince kuelekea kwenye mabaki ya meli ya Titanic mita takriban 3,800 chini ya bahari. Wafanyakazi walipoteza mawasiliano na chombo hicho karibu saa moja na dakika 45 kikiwa ndani ya maji. Waliandika kwenye Twitter kwamba utafutaji wa chombo hicho umeanza.

**Juni 21:** Walinzi wa Pwani wa Marekani waliandika kwenye Twitter kwamba ndege ya Canada iligundua kelele za chini ya maji katika eneo la utafutaji ambazo zilisababisha shughuli za gari zinazoendeshwa kwa kiongoza mbali (ROV) kuchunguza kelele


Meli Atlantiki ya Kaskazini ziliendelea kutafuta na kelele za kishindo ziligunduliwa

**Juni 22:** Mabaki yaligunduliwa na ROV karibu na ajali ya Titanic. Mkia wa nyambizi Titan ulipatikana futi 1,600 (mita 488) kutoka upinde wa Titanic kwenye sakafu ya bahari.

OceanGate ilitoa taarifa iliyothibitisha kwamba Mkurugenzi Mtendaji Stockton Rush, Shahzada Dawood, na mtoto wake Suleman Dawood, Hamish Harding na Paul-Henri Nargeolet, walifariki katika ajali hiyo.


Suleiman Dawood.


Stockton Rush.


Nyambizi ya Titan.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**OMARY ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P1378/0811 kilichotolewa na **CENTRE YA CHUO CHA UALIMU KLERUU** mwaka **2008.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/212827/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya......SENGEREMA**
**Kituo cha..........NYEHUNGE Mkoa.........MWANZA**
**Shauri la ndoa na 13,2023**
**Jina la Mdai : LILIAN AMRI AYUBU**
**Jina la mdaiwa: EDIGA THEOBADI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa, EDIGA THEOBADI WA MISENYI- BUKOBA- KAGERA**
Kwa kuwa mdai/ wadai ameleta/ wameleta madai yake/ yao kwamba(Eleza hapa habari za madai)
**KUOMBA KUPATIWA TALAKA.** Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 27 mwezi wa 06 mwaka 2023 saa 09:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa Amri na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 22 mwezi 06 mwaka 2023.

HAKIMU
.................................
**HAKIMU**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 178 YA 2023**
**MUSSA JOHN KAMOTA ............MDAI**
**VERSUS**
**STELLAH AINEA ...............MDAIWA 1**
**BARK ZACHARIA...............MDAIWA 2**
**CHISTINA ZEBEDAYO ZEFANIA............MDAIWA 3**
**MZEE CHIUYO............MDAIWA 4**
**ABUSHIRI SEIF ABUSHIRI.........MDAIWA 5**
**MWANTUMU ABDALLAH.........MDAIWA 6**
**KWA:**
**STELLAH AINEA**
**BARK ZACHARIA**
**CHISTINA ZEBEDAYO ZEFANIA**
**MZEE CHIUYO**
**ABUSHIRI SEIF ABUSHIRI**
**MWANTUMU ABDALLAH**

**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.07. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 22 ya mwezi wa SITA, 2023.

**SHAURI JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ......TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi Na...111.../2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MICHAEL TARUMBETA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: RESTITUTA DAVID SHANGAWALE**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 27 mwezi 6 mwaka 2023 kabla, huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leoTarehe ....21... mwezi ...6...mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU MWANZO
MAHAKAMA MJINI TANGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MADAI NAMBA 22, 2021**

**JUMA LUKINDA MAJEGELO........MDAI**
**DHIDI**
**PATHEC LIMITED...........MDAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**PATHEC LIMITED**

**POPOTE ULIPO**

Unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya ya Morogoro tarehe 28 Mwezi 6 Mwaka 2023 Saa 2:30 Asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa.

Endapo hutofika wewe binafsi ama Mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

**Imesainiwa leo tarehe 22 Mwezi Juni Mwaka 2023.**

MOROGORO.

## MNADA WA HADHARA

**RAISSA COMPANY LIMITED na WHITE MIRACLES (T) LTD** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na minada ya hadhara ya kuuza dhamana za wadaiwa sugu kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.Minada itaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Biswaro Zebedayo Msase | Nyumba- Mtaa Mloganzila- Kwembe - Dsm | 30 June 2023 | RAISSA CO. LTD |
| Omary Bakari Wachopa | Nyumba- ipo Churwi, Kijiji cha Mlamleni (MKURANGA) | 07 July 2023 | WHITE Miracles Ltd |

**Masharti Mengine:**

Minada itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.

Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**RAISSA Company Ltd:**
**0652113262/ 0757433333**
**WHITE MIRACLES LTD: 0684937219**


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-14

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Eddy huwa na watu wake wa karibu ambao huwatumia kwenye kazi zake, lakini amekuwa akiwatumia kupata taarifa sahihi, lakini hawapi kwa undani kabisa ni nini anachotaka kukifanya. Anaweza kuwapa kazi ya kumfuatilia mtu fulani au kitu fulani ili atumie mrejesho, lakini watu hawajui huyo mtu amefanya nini na sababu gani.


Rashid ni mmoja kati ya rafiki zake na watu wake ambao huwatumia sana. Ni mfanyakazi wa serikali ambaye yupo Dodoma kwa miaka miwili sasa.

Kile alichokuwa akikidhani, au kukifikiria kilianza kuonyesha mafanikio. Moja ya maelezo aliyoyapata kwa mjomba wa Tessy, alivutiwa na majina kadhaa aliyoyaulizia kiujanja. Akaanza kuyafanyia kazi. Akawa na wasiwasi na jina la mtu mmoja hivi. Alichofanya ni kuchunguza nyendo zake. Ndiyo akampa kazi Maria, mfanyakazi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage Nyerere.

Aliyemshuku ni huyu mfanyakazi wa Maliasili. Akapata taarifa zake kuwa anafanya kazi Dodoma, lakini mara kwa mara huja Dar es Salaam.

Safari zake zote alizotumia ndege ni kutoka Dar kwenda Dodoma kikazi na kurejea. Ni mara moja tu alitoka Mwanza kwa ndege kuja Dar na kesho yake akaenda Dodoma. Sasa kwa mujibu wa Rashid ni kwamba alikuwepo kwenye semina iliyoandaliwa kwa watumishi wa Maliasili. “Walitoka Dodoma kwa basi na walirudi kwa basi. Lakini huyu jamaa alipanda ndege na kurudi Dar, akiwaacha wenzake wakipumzika siku moja baada ya siku tatu za semina. Akaja kwa siku moja tu, kesho yake akaondoka kwenda Dodoma, siku ambayo wenzake nao walikuwa wanarejea. Kwa bahati mbaya sana, siku hii ambayo anatua mchana Dar, ndiyo siku ambayo mjomba wa marehemu Tessy anasema hakurejea nyumbani na maiti kuonekana siku tatu baadaye.” Eddy alijisemea mwenyewe.

Kama kawaida yake, huwa na tabia ya kutaka kupata ushindi pasipo shaka ili hata kama anamtia hatiani mtuhumiwa, basi hata kama anapelekwa mahakamani hawezi kuruka kwani kila kitu kinakuwa mkononi mwake. Na hiyo ndiyo sifa kubwa ya Eddy Kamal. Kuja Dar pekee na kuwa ndiyo siku ambayo marehemu hakurejea nyumbani hakuwezi kumfanya hakimu kuthibitisha kuwa atakuwa ndiye aliyemuua Tessy. “Bado kuna vitu vinahitaji kufanyika.” Akajiambia.




**“Samahani Maria, leo nina kazi nyingi sana, naomba unisaidie kitu kimoja tu.”**

Akampigia tena simu Rashid.

“Samahani, nimekuingizia pesa za usumbufu kidogo kwenye simu yako, kuna risiti huku zimeletwa zinatupa ukakasi kama zingine ni feki. Sasa ninachoomba wewe unitafutie majina ya watu ambao hawakupanda basi wakati wa kurudi na walisalia wapi, kama walishukia njiani kwenda kusalimia kwao, au kama walibaki Mwanza, alikuwa wapi na akinanani.”

“Sawa, nimeona muamala, nitaifanya kazi hiyo kisawasawa.”

“Okay, ila usimwambie mtu yeyote kuhusu hili, maana kuna watu wezi sana, wanachukua pesa nyingi, kumbe gharama inayotumika ni ndogo.” Aliendelea kumdanganya.

Wakati Rashid akipewa kazi, akidhani Eddy anasaka waliokula pesa ya kukodisha mabasi ya kwenda semina Mwanza, kumbe yeye anataka muuaji wa mwanamama Tessy.

*****************************************

Siku tatu baadaye, tayari Eddy alikuwa amekusanya data zote ambazo alizipata akiwa amekaa ofisini tu. Kwake aliiona ni moja kati ya kesi rahisi zaidi ambazo ameshawahi kuzifanya.

Kuna baadhi ya operesheni ambazo analazimika kufanya uchunguzi wa hali ya juu. Kuna wahalifu wanaficha ushahidi kuliko kawaida. Inahitajika uwe na akili ya ziada ili kuweza kufichua hilo. Wakati mwingine hulazimika kukutana na watu wasumbufu ambao wanamfumbua kwa kumvamia kutaka kumpiga.

Yeye huwaita wasumbufu kwa sababu wanakuwa wanamchelewesha tu kufanya kazi yake, lakini hawawezi kabisa kumpiga.

Pia mara chache hukutana na operesheni au mikasa hatari ambayo inapangwa kwa watu madhubuti, wenye uwezo mkubwa, walio nyuma ya watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha, matajiri, ambao huajiri vibaraka waliomo ndani ya taasisi wanazofanyia kazi. Hawa huwezi kuuza taarifa muhimu ikiwemo hata taarifa za safari husika za mpelelezi.

Akakumbuka kwenye operesheni moja ambayo alipigiwa simu saa mbili usiku na bosi wake aende akaifanye huko Mbeya. Hakuondoka na gari lake wala la serikali, badala yake alipanda basi la abiria. Aliyemwambia ni bosi wake tu. Cha ajabu alipofika kwenye kituo cha mabasi Mbeya, alijikuta amevamiwa na watu ambao hawafahamu. Kwa sababu ni mpelelezi wa kimataifa, akili yake ikamwambia kuwa wale watu walipata taarifa kutoka vyanzo muhimu ndani ya idara yao.

Akampigia simu bosi wake na kumuuliza ni kwa nini alivamiwa na watu wanne, wakati siri ya kuondoka kwa basi anaifahamu yeye tu. Bosi akamjibu kama ni hivyo basi kuna mtu ameuza siri kwa sababu wapo aliowaambia kuwa kijana anasafiri na basi.

Eddy alimuachia kazi hiyo bosi wake na alimpata mmoja ambaye alikuwa amelipwa na matajiri waliokuwa wanataka kumzuia asiende kukomesha tukio moja la wananchi kunyang’anywa ardhi yao na kupewa mwekezaji feki.

Rashid alikuwa amemletea taarifa kuwa yule msafiri aliyepanda ndege kutoka Mwanza kwenda Dar aliwaambia wenzake kama anabaki huko kwa sababu alikuwa amepata mpenzi. Na akakodi chumba namba 210 kwenye Hoteli ya Kangaroo.

Na katika uchunguzi kwenye hoteli hiyo ilionekana walilala watu wawili mtu na mpenzi wake na aliondoka kesho yake jioni. Jina la mtu huyo ndiyo lile lile ambalo Eddy analo mkononi. Alitabasamu. Akamsifia jamaa kwa kuwa mtaalam wa kuficha ushahidi.

“Mtu huyu huyu mmoja, alibaki Mwanza wakati wafanyakazi wenzake wanarejea kazi Dodoma baada ya kumaliza semina. Akalala Mwanza kwenye hoteli ya Kangaroo, akiwa na mpenzi wake hadi kesho jioni akaondoka kurejea Dodoma na basi. Lakini mtu huyo huyo ndiye anaambiwa siku hiyo alipanda ndege asubuhi kuja Dar es Salaam na kesho yake jioni akaonekana Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere akielekea Dodoma. Akajikuta akiona kabisa kuwa hachezi na mtu wa kawaida. Japo si kivile, lakini ni mwerevu na mjanja.

Akainua siku na kumpigia Maria.

“Samahani Maria, leo nina kazi nyingi sana, naomba unisaidie kitu kimoja tu.”

“Kipi?”

“Kuna utata kidogo kuhusu hii inshu ya yule jamaa yetu wa Mwanza kuja Dar. Naona fanya kila njia unipatie video ya CCTV kamera siku hiyo anayoshuka kutoka huko, na kesho yake wakati anaondoka.”

“He, mchumba kwani huniamini siku hizi?”

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# TIMU TATU LIGI KUU ZAMTAKA MINZIRO

**Na Abdallah Mataka**

ALIYEKUWA kocha wa Geita Gold FC, Fredy Felix 'Minziro' amesema tayari amepokea ofa kutoka katika timu tatu zitakazoshiriki ligi kuu msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe, Minziro alisema amemalizana na Geita na sasa anaangalia changamoto mpya kama ataamua ni timu gani ya kujiunga nayo kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu.

Alisema mpaka sasa klabu za Namungo FC, Mbeya City na Tabora United (Zamani Kitayose FC) zote zimeonyesha nia ya kumtaka kwa ajili ya msimu ujao.

"Bado sijasaini mkataba na timu yoyote, hizo zimeonyesha nia, napumzika kwa muda baada ya hapo mtajua wapi naenda kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu," alisema Minziro.

Hata hivyo alisema Tabora United imeonyesha nia kubwa zaidi ya kutaka kumpa kazi ya kuifundisha timu hiyo iliyopanda daraja kushiriki ligi kuu msimu ujao.

Alisema ana uhakika msimu ujao atakuwa na timu ya kufundisha ligi kuu na mambo yatakapokamilika atatangaza timu gani anaenda.

Minziro ni mmoja kati ya makocha wazawa waliopandisha daraja vilabu vingi kucheza Ligi kuu akifanya hivyo katika vilabu vya Geita Gold, Singida United na KMC na kuwa miongoni mwa makocha wazawa waliopandisha timu nyingi Ligi Kuu.



Mchezaji wa Timu ya Mpira wa Kikapu ya Rwanda, Obsom Shema (kushoto), akitoa pasi huku mchezaji wa Burundi, Steve Nsumizi (katikati), akizuia wakati wa michuano ya kufuzu Fiba Afrocan inayoendelea katika Uwanja wa Ndani wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. Burundi ilishinda 53-52. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mabondia watakiwa kuchangamkia Bima za Afya

**Na Saada Akida**

MABONDIA nchini wametakiwa kuchangamkia Bima za afya ili kuwa na uhakika wa matibabu pindi wanapoumwa au kupata majeraha wanapokuwa kwenye mapambano ulingoni.

Ushauri huo umetolewa na bondia wa ngumi za kulipwa nchini Seleman Kidunda wakati wa zoezi la kupima afya kwa mabondia watakaopanda ulingoni Juni 30 katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam.

Kidunda, mwajiriwa wa jeshi la wananchi la Tanzania (JWTZ) anajiandaa kupanda ulingoni siku hiyo kupigana na Erick Mukadi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Congo (DRC).

"Bima za afya ni jambo la msingi kwa mabondia kwa sababu unapopanda ulingoni kunakuwa na mambo mawili, kupigwa na kupata majeraha japokuwa hatuombei suala hilo kutokea, lakini utahitaji matibabu ukishuka ulingoni, na pia itamsaidia katika maisha ya baadae tunapokuwa tumestaafu mchezo huu," alisema Kidunda.

Alisema bondia kuwa na bima ya afya kunasaidia kupunguza gharama za fedha ambazo angetakiwa kujihudumia.

"Mabondia wenzangu wawe na bima za afya itawasaidia sana, pia ni muhimu hasa kutokana na kazi zetu, "alisema Kidunda.

Kuhusu maandalizi ya pambano lake, Kidunda alisema yupo tayari kwa pambano hilo na amejiandaa kwa ajili yakushinda na sio vinginevyo.

"Nimejiandaa vizuri mpaka sasa, nina afya nzuri na nategemea pambano litakuwa zuri sana, nahitaji kuwafurahisha Watanzania nataka kufanya kitu watu wafurahi na wapate burudani maana mchezo wa ngumi ni mchezo wa burudani, waje waangalie Kidunda anafanya kitu gani," alisema Kidunda.

Katika pambano hilo litakalofanyika Jumamosi ijayo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma (Mwana FA) pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila.

## *Ihefu yawatoa hofu mashabiki wake*

**Na Abdallah Mataka**

UONGOZI wa klabu ya Ihefu FC umewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kutokana na ukimya wao kwenye kipindi hiki cha usajili na kusema wanafanya mambo yao kimyakimya na watakapokamilisha watawatangaza wachezaji wanaoachwa na wale watakaowasajili.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasilino wa Klabu hiyo, Peter Andrew alisema, hawafanyi mambo yao kwa kukurupuka wala kwa mihemko hivyo mashabiki wao wanapaswa kuwa watulivu na wakati wowote Uongozi utaweka wazi kila kitu.

Andrew alisema Uongozi wao kwa sasa unaendelea na vikao vya ndani sambamba na kupitia ripoti ya benchi la Ufundi ambayo yenyewe ndio itatoa muongozo wa kuachwa kwa Wachezaji na wale watakaosajiliwa kwa ajili ya msimu ujao wa 2023/2024.

"Uongozi wetu unaendelea na vikao vya ndani kwa ajili ya kupitia ripoti ya benchi la Ufundi, nina uhakika kwa asilimia 100 ripoti itatoa muongozo wote wa wanaoachwa na watakaosajiliwa, kwa hiyo tusubiri kila kitu kitawekwa wazi" alisema Andrew.

Kuhusu tetesi za baadhi ya nyota wake kutakiwa na timu nyingine kwa ajili ya msimu ujao, Andrew alisema wanasubiri kumaliza kupitia ripoti ya mwalimu kufahamu wachezaji gani watakuwa nao na wachezaji gani watawaacha.

Wachezaji Nicholus Wadada na Yahaya Mbegu wanahusishwa kutaka kujiunga na klabu ya Singida Fountain Gate.

"Ni kweli wachezaji hao mikataba yao imefika mwisho hivyo tunasubiri kumaliza kupitia ripoti ya kocha kujua kama alikuwa anawahitaji tutakaa nao mezani kufanya mazungumzo ya kuongeza mkataba kama ataona waende basi wataenda wanapotaka kwenda," alisema Andrew.

Alisema baada ya kupitia ripoti hiyo na kujua matakwa yake, wataanza mchakato wa kukiimarisha kikosi hicho na kuanza maandalizi kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu.

## Wakimbiaji 1,500 kushiriki 'Run for Binti Marathon'

**Na Frank Monyo**

ZAIDI ya wakimbiaji 1500 wanatarajiwa kushiriki katika mbio za marathoni za 'Run For Binti Marathon 2023' zitakazofanyika Julai 30 Jijini Dar es Salaam zikiwa na lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya kuwawezesha watoto wa kike kupata taulo za kike.

Mbio hizo ambazo awali zilikuwa zifanyike Julai 2 kabla ya kupelekwa mbele mpaka Julai 30 zinaandaliwa na Shirika la sheria la ' Legal Services Facility' (LSF) kwa kushirikiana na Shirika la Smile for Community (S4C) ambapo zaidi ya washiriki 1,500 watashiriki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa S4C, Flora Njelekela alisema mbali na mabadiliko ya tarehe za mbio hizo, LSF na S4C wanayofuraha pia kuzindua jezi mpya kwa ajili ya mbio zilizobuniwa kwa ubora mzuri na kumfanya mshiriki ajisikie amani wakati wote wa mbio.

"Lengo la mbio hizi ni kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya kuwezesha watoto wa kike kupata taulo za kike ili kuboresha upatikanaji wa haki ya afya ya uzazi hususani hedhi salama na safi pamoja na kuboresha mazingira bora na rafiki katika sekta ya elimu kwa mtoto wa kike yatakayomuwezesha kupata hedhi iliyo salama kupitia ujenzi wa miundombinu bora hususani vyoo," alisema Flora.

Aidha aliitaja mikoa ambayo itanufaika na mbio hizo kuwa ni Mtwara na Lindi, ambapo watoto wa kike kwenye shule za sekondari watapatiwa bidhaa za hedhi salama na uboreshwaji wa miundombinu hususani vyoo salama.

"Sambamba na hilo vikundi vya wanawake vya kiuchumi katika ngazi ya jamii vitawezeshwa kwa kupatiwa mashine na vitambaa maalumu vitakavyowawezesha kushona sodo (taulo za kike) na kuziuza kwa bei nafuu kwenye shule mbalimbali na hivyo kujiinua kiuchumi," alisema.

Aidha, Flora aliwashukuru wadau wote waliowaunga mkono katika kufanikisha mbio hizo ambao ni TotalEnergies,Dar Fresh Care kupitia bidhaa yao ya Afya water,Tips na SGA Security Company.

Meneja Rasilimali na Mawasiliano kutoka LSF, Jane Matinde aliwashukuru wadau ambao wameweza kuona umuhimu wa mbio hizo na kuweza kujitolea ili kuendelea kufanikisha tukio hilo la kijamii.

"Naomba tujumike pamoja kama jamii na tuhamasishe wengine na tuonyeshe nguvu ya pamoja katika kujitolea. Kwa michango yenu tunaweza kuleta matokeo chanya kwa mustakabali wa watoto wa kike nchini, tukielekea Julai 30 nawaomba wadau wote kushiriki mbio hizi kwa ajili ya kumuinua mtoto wa kike," alisema Jane.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**MO ATAKIWA ARABUNI**
MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, ndiye mchezaji mwingine anayesakwa na Ligi Kuu ya Saudia baada ya kuwasili kwa Karim Benzema na N'Golo Kante. (*Four Four Two*)

**KLOPP HANA MPANGO**
WAKALA wa Jurgen Klopp amepuuzilia mbali tetesi kwamba kocha huyo mkuu wa Liverpool anaondoka Anfield kwenda kuchukua mikoba ya Hansi Flick kama kocha wa timu ya taifa ya Ujerumani. (*Mirror*)

**LUKAKU AWANIWA**
AC Milan inatumaini kuwashinda mahasimu wao Inter Milan katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30. (*Gazzetta dello Sport*)

**MOUNT KUUZWA**
KLABU ya Manchester United imeafikiana na Chelsea kuhusu dili la la kumsajili kiungo wa England, Mason Mount, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 akikaribia kununuliwa kwa pauni milioni 60. (*Mirror*)

**RICE KUWA NAHODHA**
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anaamini kuwa kiungo wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24 ndiye nahodha wa baadaye wa klabu hiyo na Washikabunduki wanajiandaa kuwasilisha ofa ya tatu hivi karibuni na mahitaji mengine ya West Ham. (*Mail*)

**RICE HAITAKI CITY**
DECLAN Rice bado ana nia ya kujiunga na Arsenal licha ya Manchester City kuonesha nia ya kujiunga na kinyang'anyiro hicho na washindi hao wa mataji matatu pia wanaweza kukidhi bei ya pauni milioni 100. (*Guardian*)

**MADDISON AWINDWA**
KLABU ya Tottenham Hotspur imeibuka kuwa mstari wa mbele kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na England, James Maddison mwenye umri wa miaka 26. (*Guardian*)

**WALKER MIAKA MIWILI**
KLABU ya Bayern Munich iko tayari kumpa mkataba wa miaka miwili beki wa kulia wa Manchester City na England, Kyle Walker mwenye umri wa miaka 33. (*Bild*)

**JAMES AWANIWA FULHAM**
KLABU ya Fulham inaongoza kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa Southampton na England, James Ward-Prowse, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 akiwa tayari kuhamia pale Craven Cottage baada ya timu hiyo kushuka daraja kutoka Ligi Kuu. (*Independent*)

**MEJBRI ATAKIWA**
KLABU ya Borussia Dortmund inapanga kutoa kitita cha pauni milioni 13 kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United na Tunisia, Hannibal Mejbri mwenye umri wa miaka 20, ambaye msimu uliopita alichezea Birmingham kwa mkopo. (*Manchester Evening News*)

**BEEK NA ROMA**
KLABU ya Manchester United imeipatia AS Roma nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 26. (*Metro*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RICE AZIGONGANISHA MAN CITY, ARSENAL

### Kuondoka kwa Gundogan kwa kwaifanya City kumfuatilia kiungo huyo....

**LONDON,** England

MANCHESTER City inajiandaa kushindana na Arsenal katika mbio za kumsajili Declan Rice kwa kutoa ofa rasmi kwa kiungo huyo wa kati wa West Ham United, vyanzo vimeiambia ESPN.

**City wamekuwa wakifuatilia maendeleo huku Arsenal ikikataliwa ofa mbili za kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 mapema mwezi huu, ambapo ofa za hivi punde zilifikia pauni milioni 90.**

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba City walikuwa wanamngoja Ilkay Gundogan kuamua mustakabali wake kabla ya kuhamia kwa kiungo mpya, na sasa kwa kuwa amechagua kukataa mkataba mpya wa kujiunga na Barcelona, kikosi cha Pep Guardiola kiko tayari kuchukua hatua.

West Ham wamemthaminisha Rice kwa zaidi ya pauni milioni 100 na Arsenal wanatarajiwa kurejea na ofa ya tatu. Inabakia kuonekana ni kiasi gani City wako tayari kutoa zabuni lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu England wakiashiria nia yao huenda wakaongeza ada hiyo.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Arsenal walikuwa na uhakika kwamba Rice alitaka kuhamia pale kwenye dimba la Emirates, lakini City itajaribu kujiamini, hasa ikizingatiwa kuwa wanaweza kuwajaribu West Ham kwa dili la mchezaji pamoja na fedha.

Kocha wa West Ham, David Moyes anafikiriwa kuwa shabiki wa kiungo wa City, Kalvin Phillips. Ikiwa Rice ataamua kujiunga na City, Phillips atakuwa nyuma yake na Rodri katika mpango wa kuanza.

Phillips anasita kuondoka na atalazimika kushawishika kuwa hana mustakabali wa klabu hiyo ili kuendelea na soka lake kwingine.

Arsenal wamemfanya Rice kuwa mlengwa wao mkuu wa safu ya kati na waliamini kuwa mazungumzo yanaendelea vizuri huku maslahi binafsi hayafikiriwi kuwa tatizo.

## Klopp hana mpango na timu ya taifa

**MUNICH,** Ujerumani

JURGEN Klopp hayupo kwenye kinyang'anyiro cha kuwa kocha mkuu wa Ujerumani hivi karibuni kufuatia ombi kutoka kwa vyombo vya habari vya nchi hiyo kumtaka kuchukua nafasi ya Hansi Flick.

Ujerumani ilipokea kichapo cha mabao 2-0 nyumbani kutoka kwa Colombia mapema wiki hii.

Ujerumani sasa wana mechi nne bila ushindi - ushindi wao wa mwisho ulikuwa dhidi ya Peru Machi - huku wakiwa wameshinda mechi tatu pekee kati ya 11 zilizopita.

Kiwango hicho kibaya kinajumuisha mechi za kufuzu kwa hatua ya makundi katika Kombe la Dunia la 2022 kwa mchuano wa pili mfululizo.

Kwa matarajio ya Ujerumani kufanya vyema kama waandaji wa Euro 2024 msimu ujao wa joto, imeweka shinikizo kubwa kwa kocha wa zamani wa Bayern Munich, Flick kubadili mambo.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 58 aliajiriwa kuchukua nafasi ya bosi wa muda mrefu Joachim Low mnamo 2021 na anaweza kukabiliana na kufutwa kazi bila kuimarika kwa haraka.

Klopp ndiye kocha wa Ujerumani mwenye hadhi ya juu zaidi katika kandanda ya dunia na ndiye anayetajwa sana kupewa kazi hiyo.

Baada ya ombi la wanahabari kwa chama cha soka cha Ujerumani, DFB, kukata Klopp ampewe nafasi hiyo, wakala wake amejibu na kusema hawezi kuchukua nafasi hiyo

"Jurgen ana mkataba wa muda mrefu na Liverpool na DFB ina kocha. Hii sio mada kwetu hata kidogo," alisema Marc Kosicke wakala wa Klopp akiwaambia waandishi wa habari jana.






# NAHODHA REAL MADRID MKATABA MPYA

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imethibitisha kuwa nahodha wake, Nacho Fernandez amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja katika klabu hiyo.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 33 alitangaza mapema mwezi huu kwamba ameamua kukubali ofa ya Madrid ya kumpa mkataba mpya, baada ya hapo awali kufikiria kuondoka katika klabu hiyo ili kutafuta nafasi zaidi ya kucheza.

Taarifa ya klabu ilisema siku ya Alhamisi: "Real Madrid na Nacho Fernandez wamekubali kuongeza mkataba wa nahodha wetu, na kumfanya ajiunge na klabu hadi Juni 30, 2024.

"Nacho ameiwakilisha Real Madrid kwa miaka 22, tangu ajiunge na akademi ya vijana chini ya umri wa miaka 11 mnamo 2001.

"Amecheza mechi 319 katika kikosi cha kwanza cha Real Madrid, akishinda mataji 23, Mataji matatu ya Ulaya, matano ya Ligi ya mabingwa Ulaya, matatu ya Uropa, matatu ya LaLiga, mawili ya Copas del Rey na manne ya Super Cup."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania Nacho amechukua nafasi ya nahodha wa klabu tangu kuondoka kwa Karim Benzema mapema mwezi huu.

"Siku zote kuna ofa kutoka mahali pengine, lakini nimeamua kubaki kwa mwaka mmoja zaidi,"alisema Nacho akiiambia TVE Juni 11.

"Nina furaha sana na nina furaha ya kukaa."

Beki huyo mwenye uwezo mkubwa, ambaye nafasi yake anaipenda zaidi ni beki wa kati lakini pia anaweza kucheza kama beki wa pembeni kila upande, amewaacha Eder Militao, David Alaba na Antonio Rudiger miongoni mwa chaguzi za kocha Carlo Ancelotti katika safu ya ulinzi ya kati.

Nacho alicheza mechi 27 za LaLiga msimu uliopita, akianzia 18 kati ya hizo, lakini alizidi kuwa muhimu katika kipindi cha kampeni jambo ambalo lilimshawishi kuendelea Bernabeu.

## *Bale: Messi ataenjoi sana Marekani*

**LONDON,** England

GARETH Bale amesema Lionel Messi atakuwa na presha ndogo ya kushinda katika Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS, kwa sababu klabu za huko "zinakubali kupoteza ."

Mapema mwezi huu, Messi alitangaza kuwa ana nia ya kujiunga na klabu ya Inter Miami baada ya kuondoka Paris Saint-Germain, ingawa dili bado halijakamilika.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2022 alihusishwa na kurejea katika klabu yake ya zamani ya Barcelona lakini aliamua kuhamia Marekani na kusema alitaka kufurahia soka lake "kwa njia ya utulivu."

Barca ilikubali uamuzi wa Messi kwa kutoa taarifa ikisema alichagua "kushindana katika ligi yenye mahitaji machache."

Bale, ambaye alimaliza maisha yake ya uchezaji katika klabu ya LAFC, alikubali kwamba Messi angefurahia maisha rahisi nchini Marekani bila kuangaziwa mara kwa mara kushinda kila wiki.

"Imepoa zaidi," alisema Bale akiiambia BT Sport.

"Ukishindwa ukiwa Real Madrid, ni kama ulimwengu umekwisha, umesulubishwa. Unajisikia vibaya. Unarudi nyumbani na huna furaha.

"Wanakubali kupoteza zaidi (katika MLS). Hakuna matokeo. Huwezi kushuka daraja hapo hapo. Unapopoteza mchezo unakwenda kwenye mchezo unaofuata. Wanakubali kupoteza zaidi hapo.

"Wanajua jinsi ya kupoteza lakini wanasherehekea kila ushindi kama vile umeshinda ubingwa. Hakika atafurahia."



Mwaka jana kabla ya kutangaza kustaafu, Bale alijiunga na LAFC kwa mkataba wa miezi 12 na kuisaidia kupata taji lao la kwanza kuu kwa kuishinda Philadelphia Union kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya Kombe la MLS.

Mapema wiki hii, mmiliki wa Inter Miami, Jorge Mas aliwaambia waandishi wa habari kwamba klabu hiyo inapanga Messi kucheza mechi yake ya kwanza Julai 21 katika mechi ya Kombe la Ligi dhidi ya Cruz Azul wa Liga MX.

HABARI MICHEZO

# AZAM YAMKANA MTUKUTU MORRISON, YAMUONGEZEA MKATABA AKAMINKO

**Na Adam Fungamwango**

AZAM FC imekanusha tetesi zinazodai wapo mbioni kutaka kumsajili winga aliyeachwa na klabu ya Yanga, Bernard Morrison, huku ikimuongezea mkataba wa miaka miwili kiungo wake tegemeo, James Akaminko raia wa Ghana.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema jana kuwa Morrison hayumo kwenye orodha ya wachezaji wanaotakiwa na klabu hiyo kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu.

**Popat alisema baada ya kumsajili kiungo mshambuliaji Feisal Salum 'Fei Toto', wa natarajia kusajili wachezaji wa kigeni wawili au watatu kwenye nafasi amba zo zimeelekezwa na benchi la ufundi**

"Katika wachezaji wanaokuja Morrison hayumo." alisema kwa kifupi Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Hata hivyo aliainisha nafasi ambazo watazijaza kuwa ni beki wa kushoto, mshambuliaji mmoja na kiungo mshambuliaji mmoja.

"Msimu uliopita tulisajili wachezaji sita wa kigeni na wa ndani tisa kwa hiyo kikosi tunacho na kinajitosheleza, kilichopo ni kuongezea mapengo machache yaliyopo kama benchi la ufundi lilivyopendekeza na tutakuwa na maingizo ya wachezaji wa kigeni wawili, wakizidi sana watatu, kama ulivyoona beki wetu wa kushoto Bruce Kangwa ameondoka, hapo ni lazima tuingize mwingine na mbele pale tutasajili straika mmoja na kiungo mshambuliaji," alisema Popat.

Katika hatua nyingine, Klabu hiyo juzi usiku ilitoa taarifa ya kumuongezea mkataba Akaminko kuendelea kusalia kwenye viunga vya Chamazi siku moja tu baada ya kumuongezea mkataba kiungo mkabaji mwingine, Sospeter Bajana.



Mchezaji wa Netiboli wa timu ya Upendo Queens, Hellen Matiko, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa NSSF wakati wa michuano ya mchezo huo ligi daraja la kwanza katika viwanja vya Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam jana. NSSF ilishinda 67-15. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mayele safi, Wakongo wengine waiwekea ngumu Yanga SC*

INATOKA UK 24

"Hii inatokea pale timu inapofanya vizuri hasa kwenye mashindano ya kimataifa, na kama unavyojua wachezaji hiki ndio kipindi chao cha kuvuna, lakini Yanga kama Yanga tunaendelea na juhudi za kuwabakisha wachezaji wote ambao tunawahitaji," alisema.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema uongozi unaendelea kufanya tathimin ya msimu uliopita na kujua wapi wanatakiwa kufanya marekebisho.

Alisema kama kuna mchezaji au mfanyakazi mwingine yeyote atataka kuachana nae au kuboresha maslahi watakubaliana kwa utaratibu na kumaliza jambo hilo salama.

Hadi sasa Yanga imetangaza kuachana na wachezaji watatu, Benard Morrison, Tuisila Kisinda na Dickson Ambundo.



# Huyu hapa mrithi wa Kakolanya Simba

**Na Saada Akida**

SIKU chache baada ya Uongozi wa Simba kutangaza kuachana na kipa Beno Kakolanya aliyemaliza mkataba wake, tayari majina mawili yameanza kujadiliwa ili mmoja wapo kuchukua nafasi ya kipa huyo aliyetimkia Singida Fountain Gate.

Magolikipa wanaojadiliwa mmoja wapo kuchukua nafasi ya Kakolanya ni golikipa wa Al Hilal ya Sudan, Issa Fontana pamoja na golikipa wa Vipers ya Uganda, Alfred Mudekereza.

Inaelezwa majina hayo ni mapendekezo ya kocha wa timu hiyo Robert Oliviera 'Robertinho' ambaye ameomba uongozi uangalie uwezekano wa kumsajili mmoja kati ya magolikipa hao ili kumsaidia golikipa namba moja, Aishi Manula.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu alisema baada ya kuachana rasmi na kipa wao Kakolanya na kwenda kutafuta changamoto nyingine wako katika mchakato mzuri wa kupata mbadala wake na mambo yanaenda vizuri.

Alisema wanahitaji kufanya maboresho makubwa ndani ya kikosi chao na kukisuka vizuri kwa kufanya usajili kulingana na mapendekezo ambayo ameyatoa kocha Robertinho ili kuwa na kikosi imara.

"Kuhusu golikipa utaratibu unaendelea, yapo majina tunayoyajadili na utafanyika usajili mzuri kwa kuzingatia mahitaji ya benchi la ufundi, tutampata kipa mzuri zaidi kati ya majina haya yaliyopo mezani kwetu, kwenye usajili hatutaki kurudia makosa tuliyoyafanya kwenye msimu uliopita," alisema Mangungu.

Golikipa namba moja wa timu hiyo, Manula atakuwa nje ya Uwanja kwa miezi mitatu na anatarajiwa kurudi Uwanjani Septemba mwaka huu baada ya kufanyiwa upasuaji wa nyama za paja mwezi uliopita Afrika Kusini.

## Mkude azungumza kwa uchungu akiaga Simba


INATOKA UK 24

"Mwisho wa siku Mungu ndiyo kila kitu, aliniweka kwenye kipindi chote tukishirikiana, nimecheza kwa mafanikio japokuwa siyo makubwa sana kihivyo, najivunia kuwa ni mchezaji niliyedumu muda mrefu Simba nikiwa mdogo, nimeingia hapa mwaka 2011 mwezi Oktoba naishukuru menejimenti nzima, wanachama na mashabiki wa klabu, nawaambia tutaonana wakati mwingine," alisema kiungo huyo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Simba, Mangungu alisema wanamshukuru kila mchezaji aliyeachwa na timu hiyo kwa mchango wake ndani ya klabu hiyo akisisitiza wamezungumza nao wote na wameachana nao katika hali nzuri.

Wachezaji wengine ambao walitangazwa jana kuachana ni pamoja na mkongwe Erasto Nyoni aliyedumu ndani ya timu hiyo kwa miaka sita na Gadier Michael.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Juni 24, 2023



UK. 21

Rice azigonganisha Man City, Arsenal



Wachezaji wa timu ya Yanga kutoka kushoto Jesus Moloko, Fiston Mayele na Joyce Lomalisa Kwenye picha ya pamoja wakisherehekea ubingwa wa ligi kuu msimu uliopita jijini Mbeya **PICHA: MTANDAO.**

# Mayele safi, Wakongo wengine waiwekea ngumu Yanga SC

**Na Saada Akida**

## ●●● Wataka maboresho kwenye mkataba, Viongozi wapambana kuweka mambo sawa huku...

WAKATI Mshambuliaji Fiston Mayele ikielezwa amekubaliana na Uongozi wa Yanga kubaki klabuni hapo, nyota wengine kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wameiwekea ngumu timu hiyo wakitaka kuboreshewa maslahi yao ili waendelee kukipiga kwenye kikosi hicho msimu ujao.

**Inaelezwa Yannick Bangala, Jesus Moloko, Djuma Shaaban na Joyce Lomalisa wanataka waongezewe mishahara yao ku tokana na kazi kubwa waliyoifanya msimu uliopita.**

Mmoja wa viongozi wa timu hiyo aliiambia Nipashe kuwa nyota hao wapo kwenye rada za timu kadhaa za hapa nyumbani na nje ya nchi hivyo wanataka klabu yao (Yanga) iwaboreshee mishahara yao ili wabaki.

Alisema wachezaji hao msimu wa 2021/2022 ulipomalizika waliomba kuboreshewa mikataba jambo ambalo viongozi walilitimiza, na sasa wanataka wafanyiwe tena ili wabaki msimu ujao.

"Sasa hivi viongozi wanaendelea kupambana kuzungumza nao waweze kuelewana kabla ya msimu mpya haujaanza, wote bado wana mkataba hivyo mazungumzo yanaendelea, kuhusu Lomalisa ni kweli Azam FC wanahitaji huduma yake ili akachukue nafasi ya Bruce Kangwa," kilisema chanzo hicho.

Alisema Lomalisa anatakiwa na Azam FC na klabu hiyo ipo tayari kukaa meza moja na Yanga kujadiliana uhamisho wake kama watakubali kumuachia.

Kiongozi huyo alisema kuhusu Mayele tayari mambo mengi wamekubaliana isipokuwa walikuwa wakivutana kwenye muda wa mkataba ambapo klabu inataka kumpa mkataba wa miaka miwili huku mwenyewe (Mayele) akitaka mkataba wa mwaka mmoja pekee.

"Mayele asilimia kubwa atakuwepo kwenye timu msimu ujao sasa hivi vimebaki vitu vidogo tu kumalizana, kazi ipo kwa hawa wengine ambao nao wanataka maboresho," alisema kiongozi huyo.

Alisema Yanga wamejikuta kwenye majadiliano na nyota wao kutokana na kufanya vizuri msimu uliopita na kuwatangaza wachezaji wao ndani na nje ya nchi hali iliyopelekea wachezaji wengi kutakiwa na klabu nyingine.

INAENDELEA UK 23

# Mkude azungumza kwa uchungu akiaga Simba

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja baada ya Simba kutangaza kuachana na kiungo wake mwandamizi wa klabu hiyo Jonas Mkude, Mkongwe huyo ameibuka na kuaga mashabiki huku akizungumza kwa uchungu juu ya yale aliyoyapitia ndani ya timu hiyo.

Mkude alisema amedumu ndani ya Simba kwa miaka 13 akipitia nyakati zote za raha na karaha na anashukuru klabu hiyo kwa kumuibua na kumuweka kwenye ramani ya mpira mpaka sasa anajulikana.

Kiungo huyo alisema Simba ni nyumbani kwake na anaishukuru kwa kila jambo walilomfanyia katika kipindi chote akiwa mchezaji wao.

"Shukrani zangu za dhati zinaanza kwa kocha aliyekuwa kocha wangu wa timu ya vijana Selemani Matola na aliyekuwa Meneja wangu Patrick Rweyemamu wao ndiyo walioona kipaji changu na kunileta kwenye kikosi cha vijana mwaka 2011," alisema Mkude na kuendelea,

"Nilianza maisha yangu ya soka nikiwa kwenye timu ya vijana ya Simba, nilionekana na kocha Matola, na meneja ambaye amemaliza muda wake Rweyemamu, hapo ndipo safari yangu ya soka ilipoanzia, nimeichezea klabu hii kwa vipindi tofauti na nikisema hivyo siyo kama nilikuwa natoka na kurudi, hapana nimecheza kwa misimu 13 mfululizo, ila ninachokizungumza hapa ni kwamba nimecheza kwa hali zote, wakati wa shida na raha, kwa hiyo mbivu, tamu na chungu za Simba mimi nazifahamu ziko vipi, mpaka leo hii ambapo imefikia hatua mimi mkataba wangu umekwisha," alisema Mkude.

Aidha alisema anamshukuru Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed Dewji kwani alikuwa naye karibu kwa kipindi chote, lakini hakumsahau aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Geofrey Nyange 'Kaburu' kwani ndiye aliyeshinikiza kwa kiasi kikubwa yeye kupandishwa kupelekwa kikosi cha kwanza.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >